
SportPesa
TZS. 710,494,580
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Shahidi:** Nilielezwa Sabaya alipewa kazi kushughulikia wakwepa kodi Kaskazini

UKURASA 4



**Guardiola hajashtuka Solskjaer kutimuliwa**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumanne Novemba 23, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580773

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




KESI YA MBOWE

# Ni mwendo wa panga pangua

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**ADAIWA KUUAWA KIKATILI NA NDUGU**

MKAZI wa Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi aliyefahamika kwa jina moja la Mohamed maafuru Mudi, anadaiwa...

UKURASA WA 7

**PM AONYA MATUMIZI YA FEDHA ZA UJENZI**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi...

UKURASA WA 7

**EU YAUNGANISHA NGUVU KUPINGA UKATILI**

NCHI za Umoja wa Ulaya (EU) zimeunganisha nguvu katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia nchini.

**Waziri akuta kilio umeme maeneo ya wawekezaji**

UKURASA 3



UKURASA 22 2

Rais Samia Suluhu Hassan akimtunuku kamisheni mmoja wa maofisa wanafunzi kundi la 02/18 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika sherehe zilizofanyika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli mkoani Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Samia atunuku 118 kamisheni Uluteni Usu chuoni Monduli

**MICHEZO** AZAM WAJILAUMU WENYEWE KIPIGO KMC UK.20 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA




Uzinduzi wa mradi wa maji uliofadhiliwa na Uhuru Lions Club katika Shule ya Msingi Nyeburu iliyoko Mbuyuni Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Watatu kushoto ni Gavana wa club hiyo, Mohamed Mulla, Rais wa club, Darshan Mehta, Mwenyekiti wa Bodi wa shule hiyo, Mbita Asterius (kushoto) na Mwalimu Mkuu, Daniel Kibona.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### KESI YA MBOWE

# Ni mwendo wa panga pangua

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imetupilia mbali sababu tatu za jopo la mawakili wa utetezi kwenye kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu za kupinga kitabu cha kumbukumbu za watuhumiwa kupokelewa kama kielelezo.

Uamuzi huo wa mahakama ulitolewa jana mbele ya Jaji Joackim Tiganga, baada ya kupitia hoja za mawakili wa pande zote mbili waliokuwa wanalumbana kisheria kuhusu kitabu hicho cha kumbukumbu za watuhumiwa katika Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam (DR) kupokelewa ama la.

Kitabu hicho kilikuwa kinatolewa kama kielelezo wakati shahidi wa pili kwenye kesi ndogo, Koplo Msemwa alipokuwa akitoa ushahidi wake akieleza jinsi alivyowapokea mshtakiwa Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya Agosti 7, 2020 na kuwaweka mahabusu.

Mawakili wa utetezi wakiongozwa na Wakili Peter Kibatala, walipinga na kutoa sababu tatu ikiwamo kukiukwa kwa taratibu za kutolewa kwa kielelezo hicho.

Akitoa uamuzi pamoja na mambo mengine Jaji Tiganga alisema mahakama inajiuliza jambo la kujadili DR lilikuwa linaifikisha mahakama mwisho ama la na jibu ni hapana.

Alisema kielelezo kinaweza kutolewa mahakamani kwa utambuzi, kinapokelewa kama utambuzi ni tofauti na kinapopokelewa kwa ushahidi na kinapopokelewa kwa utambuzi mahakama inakosa hadhi ya kukitumia kama kielelezo.

"Mahakama inaona suala la kutolewa kielelezo na shahidi halikuwa linaifikisha mwisho mahakama, mahakama inakuwa imefikia mwisho ikithibitisha kwamba jambo lililoko mbele yake limeshazungumzwa na kutolewa uamuzi, jambo hilo linatakiwa liwe limemaliza kesi kwa kumkuta mshtakiwa ana hatia au kuitisha jambo lolote, amri hiyo inatakiwa iwe na matokeo ya kufikisha kesi mwisho.

"Nazingatia hoja za pande zote mbili, hakuna ubishi kwamba DRililetwa kwa utambuzi ikakataliwa sababu shahidi alishindwa kujenga msingi," alisema.

Jaji Tiganga alisema hoja iliyobakia ni kwamba kielelezo lazima kitoke kwa amri ya mahakama na imeelezwa bila kuwapo kwa amri hiyo utolewaji wa barua ya Naibu Msajili hakuwezi kuhalalisha suala hilo la utolewaji wa kielelezo.

Alisema mahakama inaona suala zima la upokelewaji wa kielelezo ni la kisheria, baada ya kielelezo kupokelewa kinabaki chini ya mahakama na kinapaswa kutolewa kwa amri ya mahakama.

"Nakubaliana na upande wa utetezi kwamba mahakama inapopokea kielelezo haihusiki na kutunza, kutunza ni jukumu la Hakimu Mfawidhi na Naibu Msajili.

"Amri inahusu kama kielelezo kinarudi kwa mwenyewe, kinaharibiwa au kinarudi serikalini, nakubaliana na upande wa utetezi kuwa Naibu Msajili hana mamlaka ya kutoa kielelezo, mamlaka yake ni kusimamia na pale kielelezo kinapokuwa katika chumba cha vielelezo.

"Kwa namna hiyo basi si kweli kwamba kielelezo hakiwezi kutolewa pasipo amri ya mahakama, hata hivyo mahakama inatakiwa ijielekeze katika sheria.

"Naibu Msajili ametajwa ana uwezo wa kutunza kielelezo kwa kesi zaidi ya moja au mahakama zaidi ya moja, kutokana na hali hiyo basi ni wazi sio kila wakati kielelezo kinapotakiwa kiwe na amri ya mahakama.

"Kielelezo kinaweza kutumika kwa kesi au mahakama zaidi ya moja bila amri ya mahakama, kielelezo sio lazima kitolewe kwa amri ya mahakama, Naibu Msajili ataandika katika kitabu cha kutoa kielelezo, kwa sababu hiyo natupilia mbali sababu zote tatu za kuzuia kupokelewa kwa DR," alisema na kupokea DR kama kielelezo cha upande wa mashtaka.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, aliendelea kumhoji shahidi Koplo Msemwa ambaye alidai katika DR aliandika alivyowapokea watuhumiwa wawili kutoka kwa ACP Ramadhan Kingai na ASP Jumanne.

Alidai alimpokea Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya na aliwaingiza kwenye kitabu hicho saa 12.09 asubuhi Agosti 7, 2020.

Shahidi alipotakiwa kuwatambua watuhumiwa hao alidai wapo kizambani na aliwatambua kwa kuwaonyesha kidole.

Upande wa Jamhuri ulimaliza kuhoji maswali kwa shahidi huyo wa pili kwenye kesi ndogo ya kupinga maelezo ya Ling'wenya kupokelewa mahakamani kama kielelezo kwa madai aliteswa, alisainishwa maelezo ya onyo kwa vitisho na hakuwahi kufikishwa Kituo cha Polisi cha Kati kama inavyodaiwa na upande wa Jamhuri.

Mawakili wa utetezi walianza kumhoji shahidi kutokana na ushahidi wake, akihojiwa na Wakili Nashon Nkungu alidai Agosti 7, 2020 kituoni kulikuwa na askari wengine zaidi ya kina Kingai.

Alidai kuwa siku hiyo hakuna mtuhumiwa ambaye alitembelewa na ndugu yake.

Akihojiwa na Wakili John Mallya kuhusu sababu ya kumtoa mtuhumiwa mahabusu, shahidi alidai alimtoa kwa ajili ya masuala ya upelelezi na sio kwenda kumpiga kama anavyodai wakili.

Akihojiwa na Wakili Peter Kibatala, shahidi alikiri kwamba vitu vilivyochukuliwa kwenye diary yake vinahusiana na kesi na ushahidi wake aliotoa mahakamani.

Shahidi alidai hafahamu kama mahakama imechukua karatasi katika diary yake kabla hajaingia mahakamani kutoa ushahidi.

Akihojiwa kuhusu DR itatambulikaje kama ya Kituo cha Polisi cha Kati, Koplo Msemwa alidai ili kukitambua lazima kisomwe ndani kwa kuwa hakuna mahali kimeandikwa Kituo cha Polisi cha Kati.

Alidai wakati anampokea Ling'wenya hakumkuta na kitu chochote na kitabu cha kumbukumbu kiliacha kutumika tangu Agosti 12, 2020.

Alidai katika kitabu hicho Adamu Kasekwa alikuwa namba 393 na Ling'wenya alikuwa namba 392, alipotakiwa kusoma namba 208, shahidi alidai haisomeki.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Kasekwa, Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanakabiliwa na mashtaka sita likiwamo la kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 5, 2020.

## Samia atunuku 118 kamisheni Uluteni Usu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu, jana aliwatunuku Kamisheni ya Uluteni Usu maofisa 118.

Kati yao 61 wa Shahada ya kwanza ya Sayansi ya Kijeshi katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli (TMA) mkoani Arusha.

Kabla ya kutunuku kamisheni, Rais na Amiri Jeshi Mkuu alikagua gwaride lililoandaliwa na maofisa wanafunzi hao.

Kati yao wanaume 99 na wanawake 19 kutoka kada za urubani wa ndege vita na Shahada ya Sayansi ya kijeshi (BMS).

Rais na Amir Jeshi Mkuu aliwapongeza wahitimu hao na kutoa zawadi kwa maofisa waliofanya vizuri akiwamo mshindi wa jumla kwa fani zote, Luteni Usu Peter Msoma.

Wengine waliopewa zawadi ni mshindi wa Medani, Luteni Usu Vivian Muchunguzi, mshindi katika taaluma. Luteni Usu Fransisco Kasongo na mshindi wa jumla kwa upande wa wanawake, Luteni Usu Yasinta Joseph.

Katika kundi la 08/2018 la Jeshi la Anga, Rais na Amiri Jeshi Mkuu alitoa zawadi kwa mshindi wa jumla wa mafunzo ya urubani wa ndegevita, Luteni Usu Emmanuel Maiumu na mshindi wa jumla kwa wanawake, Luteni Usu Judith Maghembe.

Pia, wanafunzi waliofanya vizuri zaidi katika masomo ya Shahada ya Sayansi ya Kijeshi ni Luteni Usu Fransisco Kasongo kwa upande wa wanaume na Luteni Usu Rose Temba kwa upande wa wanawake. Baada ya sherehe hizo, Rais na Amiri Jeshi Mkuu Samia alitunuku Shahada ya kwanza ya Sayansi ya Kijeshi kwa maofisa wapya 61.

Mafunzo ya Shahada hiyo yaliendeshwa Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli kwa ushirikiano na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA).

Pia Rais Samia aliwavisha Bawa la kuwathibitisha kuwa marubani rasmi wa ndege za kijeshi, Luteni Asinati Rashidi na Luteni Ibrahimu Mwamboli.

Awali, Mkuu wa Chuo cha Kijeshi Monduli (TMA), Brigedia Jenerali Jackson Mwaseba, alisema kundi cha pili la Shahada ya kwanza ya mafunzo ya kijeshi wamehitimu maofisa 75 kati yao wanawake 26 na wanaume 49.

"Katika kundi hili wanafunzi 15 tuliwaachisha mafunzo kutokana na kutofanya vizuri kitaaluma ugonjwa, utoro na utovu wa nidhamu," alisema.

Kuhusu kundi la nane la mwaka 2018 la urubani na uhandisi wa ndege, jumla ya wahitimu ni 56, mwanafunzi mmoja kati yao amepata mafunzo nchini China na katika kundi hilo wanawake ni watatu na wanaume 53.

Hii ni mara ya kwanza kwa Samia kutunuku Kamisheni katika chuo cha TMA tangu alipoapishwa kuwa Rais wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu.

Sherehe hizo zilihudhuriwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Venance Mabeyo, wakuu wa majeshi wastaafu, wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako.

Wengine ni Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani George Simbachawene na wawakilishi wa nchi marafiki.

# Waziri akuta kilio umeme maeneo ya wawekezaji

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geofrey Mwambe, amekutana na kikwazo cha umeme katika maeneo ya wawekezaji kukosa huduma hiyo wilayani Kahama, mkoani Shinyanga.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, amewasilisha kilio cha wawekezaji kwa Mwambe alipofika wilayani humo, kuwa wanakabiliwa na ukosefu wa umeme katika maeneo ya uwekezaji.

Kiswaga alibainisha hayo jana kwenye ziara ya Mwambe wilayani Kahama, alipotembelea kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi na maeneo ya uwekezaji.

Alisema katika wilaya hiyo kuna watu wenye fedha, ambao wanahitaji kuwekeza katika viwanda mbalimbali, lakini wanakumbana na kikwazo cha ukosefu wa umeme wa uhakika kwenye maeneo hayo ya uwekezaji.

"Mheshimiwa waziri, Wilaya ya Kahama tumepata wawekezaji wengi sana, wakiwamo Azam, GSM, Kom, lakini changamoto tuliyonayo ni ukosefu wa miundombinu ya umeme katika maeneo haya ya uwekezaji," alisema Kiswaga.

Kwa upande wake Waziri Mwambe alipongeza wilaya hiyo kwa kutenga maeneo na kuvutia wawekezaji, huku akizitaka taasisi za serikali zitekeleze wajibu wake.

Katika hatua nyingine, alipongeza uanzishwaji wa kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi wilayani humo, ambacho kimekuwa msaada kwao.

Aidha, alisema sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ya mwaka 2004, imedhamiria kusaidia wananchi kumiliki uchumi, katika kuongeza vipato vyao ili kuendana na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Kwa upande wake, Meneja biashara katika kiwanda cha usindikaji mazao ya chukula, utengenezaji vinywaji baridi (Kom Food product), Bryson Balemba, alisema kiwanda hicho bado hakijaanza kazi, lakini changamoto kubwa ambayo inawakwamisha ni ukosefu umeme wa uhakika.

Alisema katika kiwanda hicho, wanatarajia kutumia umeme megawati 9, ili kusukuma mashine za kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Hata hivyo, Waziri Mwambe aliahidi kwamba kero ya umeme kwenye maeneo ya uwekezaji ataishughulikia.

# Adaiwa kuuawa na ndugu, mwili wakutwa na kamba shingoni

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi aliyefahamika kwa jina moja la Mohamed maafuru Mudi, anadaiwa kuuawa kikatili na ndugu zake, huku mwili wake ukitelekezwa vichakani.

Taarifa zinadai kuwa mauaji hayo yametekelezwa na ndugu hao kwa madai ya kuhofia kutoa siri ya wizi.

Tukio hilo linadaiwa kufanyika wiki iliyopita maeneo ya Kata ya Rasbura, wakati kijana huyo na wenzake wawili, waliofahamika kwa majina ya Bakari Ally na Ramadhani, walipokwenda kuiba vifaa eneo la kituo cha Mashujaa Radio FM kinachojenga ofisi zake za kurushia matangazo.

Taarifa zilizothibitishwa na viongozi mbalimbali wa serikali, siasa na dada wa marehemu, Somoe Kitenge, zinadai kuwa wiki hiyo, Mudi alikuwa ameondoka Ruangwa kwenda mjini Lindi kumtembelea dada yake huyo.

Akithibitisha taarifa hizo, Somoe alimwambia mwandishi wa habari hizi kuwa mdogo wake alifika nyumbani kwake kumtembelea na kumueleza kuwa amekutana na vijana wenzake wawili, akiwamo mdogo wake mwingine aliyemtaja kwa jina moja la Ramadhani na Bakari Ally na kumtaka wakatembee.

Alidai kuwa katika matembezi yao walikwenda eneo ambalo kituo hicho cha radio kinajenga ofisi zake, lengo likiwa kutaka kuiba vifaa, na mlinzi aliwashtukia na kumkamata Mudi, huku wenzake wakifanikiwa kukimbia.

"Nikiwa nyumbani hapa, alifika askari na kumuulizia mdogo wangu Mudi, nikamjibu sifahamu alipo akaondoka zake," alisema Somoe.

Pia, alidai wakati askari huyo akiondoka nyumbani hapo, aliacha maagizo ya kumtaka baba wa Rama kwenda kituoni kwa maelezo kuwa kijana wake anadaiwa kushiriki wizi.

Alidai, wakati akiendelea kutafakari, alipokea simu kutoka Ruangwa ikielezea kifo cha Mudi jambo lililomfanya kuchanganyikiwa, ikizingatiwa mdogo wake huyo hakuonekana nyumbani kwa siku mbili.

Taarifa kutoka vyanzo vya habari zinadai mmoja wa watuhumiwa wa mauaji hayo alikimbia mji na kwenda kusikojulikana na ndiye inayedaiwa kupiga simu Ruangwa kuelezea kifo cha Mudi.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Rasbura, Omary Komba na Diwani Abdallah Chikwei, walithibitisha kutokea kifo hicho na mwili wake uligunduliwa kichaka cha ufukwe wa Bahari ya Hindi na watoto waliokuwa wakitafuta vyuma chakavu, ukiwa umefungwa kamba shingoni, huku ukiwa umeharibika.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi, ACP Mtatiro Kitinkwi, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alithibitisha ofisi yake kupata taarifa hiyo na kusema wanaendelea kuwatafuta watuhumiwa waliohusika na mauaji hayo.

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA YA MALIPO YA MSHAHARA KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) NCHINI TANZANIA – KUMBUKUMBU NA. 0010007291

TotalEnergies East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, Kampuni ya Mafuta na Gesi, itahitaji katika utekelezaji wake huduma ya Mkandarasi mwenye uzoefu na sifa kutoa huduma ya malipo ya mshahara. MKANDARASI atapewa jukumu la, lakini lisilojikita tu kwenye, kukusanya taarifa, maandalizi ya orodha ya wanaotakiwa kulipwa mshahara, kufanya mahesabu ya mshahara, kutoa risiti za malipo na kufanikisha shughuli zote za baada ya kufanya malipo.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania na kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Mradi wa EACOP unajiandaa kuajiri katika nafasi mbalimbali kwenye Kampuni na linahitaji usaidizi wa shughuli za Usimamizi wa Rasilimali watu kwa waajiriwa hawa.

EACOP inahitaji huduma ya malipo ya mshahara kutoka kwa mtoa huduma atakayetoa usaidizi katika kampuni kwa ajili ya kusimamia ulipaji wa malipo na matakwa ya kodi. Mhudumu atakayechukuliwa ataandaa orodha ya malipo kwa kila mwezi, atakusanya taarifa, maandalizi ya orodha ya wanaotakiwa kulipwa mshahara, kufanya mahesabu ya mshahara, kutoa risiti za malipo kwa kuzingatia usiri na kufanikisha shughuli zote zinazofuata baada ya kufanya malipo.

Mtoa huduma atakayechaguliwa atachakata taarifa za kodi na kodi za mwisho wa mwaka. Vilevile, mtoa huduma atakayetakiwa anatakiwa kuwa na uzoefu kwenye: miundombinu ya kieletroniki ya kulipa mshahara, mfumo wa kodi wa Tanzania, aweze kuzingatia sheria za nchi, viwango vya utendaji vya Kimataifa, na sheria ya ajira ya nchini Tanzania.

Mawanda yatahitaji wakandarasi kuwa na uelewa wa Mafuta na Gesi, uelewa wa kampuni ya EACOP na Mradi.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uzoefu usiopungua miaka 10 katika kutekeleza majukumu tajwa kwa uwanda mpana nchini Tanzania, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na Kimataifa.
- Idadi ya wataalam wenye vigezo na uzoefu katika maeneo tajwa.
- Uwezo wa kifedha kwa ajili ya kutekeleza mkataba.
- Uzoefu wa kuetekeleza sera husika za Ubora wa Afya, Usalama na Mazingira, utaratibu na mchakato kwa ajili ya uzabuni kwa kuzingatia viwango vya tasnia husika na vya nchi.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.
- Uthibitisho wa sera ya mkandarasi ya Ubora wa Afya, utaratibu na mchakato kwa kuzingatia viwango vya nchi na tasnia kwa kazi zinazohusiana.
- Usajili stahiki kutoka kwa mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya kutoa huduma tajwa.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **9:00** mchana Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **7 Disemba 2021.** Kichwa cha Barua Pepe ni **0010007291**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

216581702

HABARI KITAIFA



Lengai Ole Sabaya akielekea katika chumba cha mahakama.

# Shahidi: Nilielezwa Sabaya alipewa kazi kuwashughulikia wakwepa kodi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MFANYABIASHARA Francis Mroso (44), amedai kwamba alielezwa kuwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, alipewa kibali na mamlaka ya uteuzi kushughulika na watu ambao ni wakwepa kodi kwa Kanda ya Kaskazini.

Mfanyabiashara huyo, ambaye ni shahidi wa 10 wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27, inayomkabili Sabaya na wenzake sita, alitoa madai hayo, mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda, wakati akitoa ushahidi wake jana.

Sabaya na wenzake, wanakabiliwa na mashtaka matano, likiwamo la matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, kujihusisha na vitendo vya rushwa, kuongoza genge la uhalifu na kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Sylvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas, alidai ni mkazi wa Sombetini jijini Arusha na anajishughulisha na kazi ya ufundi wa magari kwenye gereji ya Mroso Injector Pump Services iliyopo kona ya Mbauda jijini Arusha, na biashara hiyo imesajiliwa TRA.

Aidha, alidai kwa kipindi chote cha biashara amekuwa mlipaji mzuri wa kodi ya serikali.

"Baada ya mteja kupatiwa huduma tunawapatia risiti za kielektroniki ya (EFD) kutoka TRA kupitia kwa wakala wao kwa ajili ya kutoa risiti, na mashine hiyo tuliipata Mei 20, mwaka 2016," alidai shahidi huyo.

Pia alidai amekuwa akitengeneza injector pumps, na wateja wake ni watu binafsi, kampuni binafsi na mashirika ya umma.

Mroso alidai Januari 22, mwaka huu, alifika kazini kwake majira ya mchana na alitoka kwenda kupata chakula na akiwa anakula, alipigiwa simu na mteja kwenda kuangali kazi akiwa ameambatana na dereva bodaboda Juma.

"Tuliondoka kwenda kuangalia kazi na niliporejea ofisini tulifunguliwa geti na niliona magari yamepaki holela likiwamo gari jeupe la serikali aina ya STL na kulikuwapo na watu wengi, wengine wakiwa ndani na nje ya ofisi.

"Nikiwa naelekea ofisini nilikuta watu wengi wakiwa ndani mmoja wa kijana aliniambia Mroso, karibu akisema wana wageni wangu na kijana huyo ninamkumbuka kwa kuwa mwaka jana Desemba alikuja kutengeneza gari katika gereji yangu," alidai shahidi.

Alidai baada ya kuingia ndani ya ofisi, aliwakuta vijana watatu wakiwa kwa karani akiwamo Sabaya, aliyekuwa amekaa kwenye kiti.

Shahidi alidai alimtambua Sabaya kwa kuwa alishawahi kukutana naye kwenye msiba kipindi akiwa Mkuu wa Wilaya na kwenye vyombo vya habari akitekeleza majukumu yake.

Alidai Sabaya alimuuliza kuwa kama ndiye Francis Mroso mmiliki wa gereji hiyo, huku akidai wanafanya kazi bila kutoa risiti na kuhujumu uchumi wa nchi.

"Nilimuuliza ni kazi gani tumeifanya bila kutoa risiti, lakini kati ya vijana wawili waliokuwapo alimtuma mmoja wa vijana aliokuwa amepatana naye ghafla aliletwa kijana mwingine ambaye awali alipeleka pumpu kutengenezwa akiwa ameshika boksi na karatasi aliyokuwa ameandikiwa gharama za matengenezo ya pampu na karani wetu.

"Sabaya alimuuliza karani wetu( Kazibira), kwamba ndiye aliyeandika gharama hizo mzee alikubali, pia alitoa simu yake na kumuonye mzee picha kwenye simu kama ni yeye na alikubali baada yule kijana kufika nilimtambua kwa kuwa Januari 20, mwaka huu alileta pampu kutengenezwa kwenye gereji," aldai Mrosso.

Alidai baada ya Sabaya kumhoji kijana huyo kwamba alipeleka pumpu hiyo kutengenezwa pale alikubali kwamba ni kweli.

"Baada ya hapo yule kijana alirudi kwenye gari na Sabaya alisema walikwenda katika eneo hilo kwa kuwa walikuwa na taarifa zake zote zikiwamo za manunuzi.

"Alimwagiza mmoja wa kijana wake kunieleza nafanyaje kazi kwa kuwa wana taarifa zangu, akidai kwamba mimi nina agiza vipuri kutoka nchi za Dubai na Kenya na kupitishia katika bandari ya Zanzibar kwa njia za panya ili kukwepa kodi na nilimkatalia, lakini alimwambia asimbishie kwa kuwa yeye ni DC.

"Aliniambia walifika pale kwa kuwa wana taarifa zangu kutoka juu na alieleza nisipotoa ushirikiano atageuka kuwa mtu mbaya kwake, kwa kuwa kutokana na taarifa hizo anatakiwa kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi kwa kukwepa kulipa kodi kutokana na kuingiza bidhaa kwa njia za panya, alidai shahidi huyo."

Alidai wakati Sabaya akizungumza mmoja wa vijana wake, aliyejifanya Ofisa wa TRA alichukua mashine ya EFD akitaka kuangalia ripoti na risiti za siku hiyo.

Alidai baada ya mazungumzo hayo, alitaka kufahamu kama nyumbani kwake kuna watu na CCTV Kamera na alimjibu kuwa kuna watu na kamera hizo.

"Aliniambia hatanifunga pingu atanipa kijana wake mmoja wa kunisindikiza ili nisikimbie, nilimjibu kwamba sina kosa la kukimbia hadi unifunge pingu.

"Baada ya hapo tuliondoka naye akiwa na vijana wake wanne na alinikabidhi kwa vijana wake wawili tukaingia kwenye gari langu nililokuwa nimepaki nje ya geti na niliwasha gari kutoka pale kuelekea Barabara ya Sombetini kuelekea nyumbani kwangu.

"Tukiwa njiani tunaelekea nyumbani kwangu mmoja wa kijana alikuwa amekaa siti ya nyuma aliniambia hii kitu imekaa vibaya na taarifa zake Sabaya alizipata kutoka juu kwenye mamlaka ya uteuzi wake.

"Aniambia ukifanya mchezo nitapotezwa na mimi nilipata hofu na alitoa simu yake akionyesha matukio ya Sabaya alivyofanya ya kukamata watu ambao ni wa uhujumu uchumi na kibali hicho alipewa na mkuu wa nchi kwa Kanda ya Kaskazini kushughulika na watu wa aina hiyo, hivyo nikifanya mchezo nitapotezwa.

"Alisema atanishauri cha kufanya huku akinieleza nifanye mpango nimwombe nizungumze naye na mimi nilimwambia anisaidie kufanya hivyo, lakini alitukana akidai kwamba Sabaya ataona kwamba walipanga naye.

Alidai alipofika nyumbani kwake wakati akitaka kushuka, mmoja wa vijana alimzuia kwenye gari huku magari mengine mawili yakimfuata na yalipofika karibu yao Sabaya alishuka kwenye gari na alimwomba kuzungumza naye.

"Alisema unataka kuzungumza na mimi, nilimjibu ndio, aliniambia kuwa hawezi kuzungumza na mimi bali atanipa vijana wake wawili na tuliingia kwenye gari kuanza mazungumzo," alidai shahidi.

## H/shauri kikaangoni kisa fedha za miradi

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameilalamikia halmashauri hiyo kwa kubakiza fedha za miradi wakati bado sehemu nyingi zikihitaji maendeleo.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2020/2021, jumla ya Sh. bilioni 1.8 zilibaki wakati bado kuna baadhi ya miradi inahitaji fedha hizo katika ukamilishwaji wake.

Hayo yalisemwa jana na diwani wa viti maalumu, Ester Matone katika kikao cha madiwani.

Ester alisema hajui ni kwa nini halmasahuri hiyo inabakiza fedha kama 'bakaa' huku bado kuna miradi mingi ya maendeleo inayozihitaji.

Akijibu hoja hiyo kwa niaba ya kamati ya fedha, uongozi na mipango, Diwani Doa Limbu alisema kuwa ni kweli fedha hizo zimebaki na hawakutarajia kuona kitu kama hicho kinaweza kutokea.

Alisema kuwa miongozo ya fedha inasema kuwa fedha hizo zinazobaki zinatakiwa kutumika ndani ya siku 90 katika mwaka wa fedha na kuongeza kuwa kama kunatokea tatizo lingine zikaenda fedha nyingi nje ya bajeti ya matumizi basi zitumike ndani ya robo ya pili.

Katika hatua nyingine katika baraza hilo, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Kahama, Mary Mhoha aliiomba halmashauri hiyo kuhakikisha asilimia 10 ya fedha za walemavu, wanawake pamoja na vijana zinatumika kama zilivyopangwa.

Alisema kuwa kama mikopo hiyo itakuwa ikitolewa kwa wakati itakuwa ikiyainua makundi hayo kiuchumi na kuongeza kuwa mshikamano kati ya watendaji na madiwani kutasaidia walengwa kufikiwa.

# TANGAZO

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

## OMBI LA KUONYESHA NIA: UTOAJI WA HUDUMA ZA URITHI WA KITAMADUNI NA AKIOLOJIA KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI.
## KUMBUKUMBU NA:10007254

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi,TotalEnergies East Africa Midstream B.V Tanzania, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma Za Urithi wa Kitamaduni na Akiolojia katika utekelezaji wa Ujezi wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la mafuta ghafi litakalofukiwa chini ya ardhi, kuanzia Ziwa Albert nchini Uganda na kuvuka mpaka hadi Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni takriban kilomita 1,443; na kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania. Bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; na pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MPANGO KAZI WA UTOAJI HUDUMA:**

Kampuni ya EACOP imezingatia Hatua Mahususi za Mradi, kufanya utafiti wa kiakiolojia na kijiolojia, juu na chini ya ardhi, katika eneo la Mradi wa bomba la mafuta, na inaendelea kufanya uchunguzi wa kiakiolojia katika maeneo hayo ili kuandaa maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa kambi za wafanyakazi na hifadhi ya mabomba (MCPY) kwa siku zijazo. Mradi unatafuta taasisi ya kitanzania yenye weledi na uzoefu na pia uwezo wa kutekeleza kazi za kiakiolojia wakati wa:

**1.** Kazi za awali za maandalizi na ujenzi wa makambi mbalimbali,

**2.** Ujenzi wa bomba la mafuta ghafi na majengo mengine, pamoja na kuchimba na kuchenjua udongo katika maeneo ambayo hayajapimwa ili kubaini uwepo wa vitu vya kiakiolojia yaliyomo ndani yake. Kazi zote za ujenzi zitatekelezwa kwa kufuata sheria za Tanzania, na viwango vya ufadhili wa kimataifa (International Financing Standards -IFS), zinazoelekeza namna ya kusimamia mambo ya urithi wa kitamaduni na kiakiolojia.

Kazi hii inahitaji mwanaakiolojia mwenye ujuzi na uzoefu mkubwa na mwenye zana na vifaa vyote muhimu vya kazi ili kutoa huduma bora za urithi wa kitamaduni na kiakolojia kwa wakati mmoja katika maeneo mbalmbali, kwa kuwahusisha wadau wa Mradi na Serikali (mfano Idara ya Malikale) kama inavyotakiwa. Huduma za Urithi wa Kitamaduni na Kiakolojia zinajumuisha uchimbaji na uchenjuaji udongo, utambuzi, kutoa muongozo juu ya usimamizi wa muongozo kuhusu hatua Mahususi za Mradi zinazoonyesha nini kitatokea katika malikale zisizotambulika, mafunzo na uhamasishaji, kuandaa nyaraka na kukamilisha kazi ya kufukua masalia katika maeneo muhimu yaliyoainishwa, ufuatiliaji, uhakiki na utoaji taarifa kwa kufuata sheria za Tanzania, viwango vya ufadhili wa kimataifa (International Financing Standards -IFS), na vigezo vya Urithi wa Kitamaduni na Kiakolojia. Kazi itahitaji kuhusisha jamii kuhusu Malikale Zinazoonekana na Zisizoonekana. Utoaji wa huduma za Urithi wa Kitamaduni na Kiakiolojia unahitaji rasilimali, na pia unaweza kuhitaji uratibu wa kazi ya kuchambua na kuhifadhi malikale, kuandaa ripoti na mikutano.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zinazotaka kuwasilisha nia zao zinaalikwa kuandika maombi yao, na kuambatanisha:

- Sifa na vyeti vya utoaji wa huduma za urithi wa kitamaduni na kiakiolijia.
- Historia fupi ya wataalamu uwa toaji wa huduma za urithi wa kitamaduni na akiolijia.
- Mifano ya uzoefu mahsusi ndani ya miaka 10 iliyopita.

**Uzoefu katika:**

- Kutoa huduma za usimamizi wa urithi wa kitamaduni na kiakiolojia..
- Ufukuaji wa masalia ya malikale ardhini.
- Uzoefu wa kazi za ujenzi na usimamizi wa muongozo kuhusu Hatua Mahususi za Mradi zinazoonyesha nini kitatokea katika malikale zisizotambulika.
- Kuandaa makabrasha na kutoa mafunzo juu ya Urithi wa utamaduni na akiolojia.
- Kufuata Kanuni na Maudhui ya Ndani, ya mwaka 2017, na sheria zinazoongoza taasisi za ndani.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za Mradi.

**Mpango wa kazi huu unaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.**

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kutuma nia zao, pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (barua pepe isizidi 20 Mb), saa **9.00** kamili alasiri au kabla, kwa saa za Afrika Mashariki (EAT), ifikapo tarehe **6 Desemba 2021.** Kichwa cha barua pepe kiwe10007254.

**Angalizo:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazowasilisha nia zao ili kupendekeza na kutengeneza orodha ya taasisi zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndizo zitakazopokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni ili kuingia katika hatua inayofuata ya mchakato wa zabuni. Maombi yote ya kuonyesha nia ya utoaji huduma yanapaswa kuandikwa kwa lugha fasaha ya Kiingereza.

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA KIBENKI NCHINI TANZANIA
## KUMBUKUMBU NA: 10007186

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma za kibenki katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Kampuni inahitaji kufungua akaunti za benki katika benki mbili za nchini Tanzania. Akaunti zitatumika kwa matumizi ya malipo ya ndani peke yake kupitia mfumo wa kuhamisha fedha kielectroniki. Malipo yatafanyika katika fedha za Kimarekani (USD) na Shilingi za kitanzania (TZS), kwa watoa huduma wengine, mamlaka za ndani pamoja na waajiriwa.

Huduma hizi hazijumuishi malipo ya nje ya mipaka ya Nchi, fedha ngumu kwa ajili ya matumizi ya dharura (Petty cash), kutoa fedha kuzidi kiwango kilichomo, mkopo, kuweka fedha, na maswala mengine ya kifedha.

Pamoja na orodha ya gharama zitakazowasilishwa na benki, watoa huduma wa ndani ndio watakaohitajika, idadi ya matawi, ushindani kwenye kubadili fedha za kigeni, usaidizi wa maswala ya kiuchumi, usaidizi katika huduma, muda wa kikomo wa siku na muda wa kukamilisha mchakato wa kazi, uwezo wa kuhudumu ndani ya tarahe iliyoombwa kwa ajili ya kufanya malipo pamoja na nafasi ya benki katika soko. Na pia utayari wa benki kushiriki katika kuwekeza fedha katika deni la nje linalotarajiwa la kibiashara.

**VIGEZO MUHIMU:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:


- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Uthibitisho wa Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mawanda ya kazi.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Inashauriwa, muoneesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **2nd Desemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe kiwe ni kumbukumbu namba husika tu. Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **10007186.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII




## Utekelezaji uonekane uondoaji wa mabondeni

**JUZI** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Willium Lukuvi, akizungumzia maendeleo ya wizara hiyo katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika, alisema serikali haitavunja nyumba zote zilizojengwa maeneo hatarishi kwa kisingizio kuwa wamiliki wake wana hati miliki za viwanja.

Alisema kwa mujibu wa sheria, shughuli za kibinadamu haziruhusiwi kwenye maeneo hatarishi kama mabondeni na kwamba yeyote atakayekaidi kwa kujenga makazi serikali itabomoa bila kujali nyaraka.

Aidha, alinukuliwa akisema miaka ya nyuma fedha ilikuwa na nguvu kuliko sheria hali ambayo ilifanya hata watumishi wa wizara kutoa hati wenye maeneo hatarishi na mabondeni kama vile bonde la Mto Msimbazi.

Pia aliwataka watumishi wa wizara kuacha kufuata hisia zao watu kwenye utoaji wa hati katika maeneo hatarishi na mabondeni. Kauli ya kiongozi huyu ni nzito na imejaa ukweli, lakini bado inatia shaka kwenye utekelezaji kwa kuwa ujenzi kwenye maeneo hayo umekuwapo miaka mingi na wizara hiyo hiyo imetoa hatimiliki kwa wahusika.

Labda waziri angedadavua kwamba miaka ya nyuma ni ipi ambayo nguvu ya fedha ilitumika kwa kuwa kuna nyakati ilifanyika bomoabomoa kuondoa waliojenga mabondeni na wengi waliondoka, huku baadhi wakifidiwa na kurudi tena kwenye maeneo hayo.

Ni kweli kuwa Mto Msimbazi ni eneo ambalo limevamiwa na cha kushangaza mamlaka nyingine kama Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), walipeleka miundombinu ya umeme. Lakini mradi wa mabasi ya mwendokasi nao ulipita eneo hilo hilo na kila wakati mvua ikinyesha Kisarawe au Dar es Saalam mawasiliano yanakatika huku vifaa vingine vikiharibika kuwa gereji ilikwenda kujengwa kwenye bonde.

Ramani ya Mto Msimbazi iko bayana na inaonyesha umbali binadamu anatakiwa kukaa lakini wameachwa na hata kumilikishwa hadi maeneo yasitostahili na hili ni tatizo la nchi nzima, ambalo linahitaji uwajibikaji kuanzia ngazi ya mtaa hadi taifa.

Kuna wakati Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), iliendesha bomoabomoa na kufanikiwa kuondoa watu katika baadhi ya maeneo, lakini kuna maeneo hayakuguswa na inapotokea mvua basi kilio ni kwa serikali.

Pia Sheria ya Mazingira inakataza shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60, lakini ukifuatilia kwa kina huko ndiko kuna shughuli za kilimo na ujenzi wa kila aina, lakini kuna mamlaka za serikali na zinaona na wakati mwingine zinahusika kutoa vibali. Ni muhimu sana kusimamia sheria zilizotungwa pasipo kuona aibu au kuweka mbele nguvu ya kisiasa, kwa kuwa madhara ni makubwa kama yanavyojitokeza kila mwaka watu kwenye mabonde na mito wanayotaabika na wote wanailia serikali.

Pia kuna haja serikali ikalisimamia hili na kukawa na uwajibikaji wa dhati kama ambavyo imewezekana kubomoa kwingine, inapotokea mtu anaanza ujenzi kwa haraka hatua zichukuliwe kuliko kusubiri amalize. Inashangaza kuwa serikali za mitaa hizo hizo ambazo zina mtu anayehusika na ardhi zinatoa ruhusa ya mtu kupewa kibali cha ujenzi kwenye eneo ambalo linajulikana kabisa haliruhusiwi.

Upo ulazima kufanya tathmini ya kina kuona ni watu wangapi wamejenga kwenye mabonde na wana hati miliki, ufanyike utaratibu wa kuzichukua kwa kuwa unapotoa hati miliki kwa mtu maana yake umeshajiridhisha na eneo husika kuwa linafaa kwa makazi ya binadamu.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



# Vikwazo kufunza TEHAMA shuleni vimejificha hapa

Na Sabato Kasika

**UJIO** wa kasi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), umeleta maendeleo katika nyanja mbalimbali zikiwamo za biashara, tiba na mawasiliano lakini kwenye elimu, imekuwa na mafanikio ya kipekee.

Ni kwasababu wanafunzi wa ngazi zozote wanaweza kutumia simu na kompyuta popote walipo ikiwa kuna mtandao, kujifunza na kujiongezea maarifa.

Hili linawezekana bila kujali uko kijijini au kwenye majiji makubwa, bora tu kuwe na umeme na 'Wi-Fi' au mtandao wa intanet usiotumia nyaya unaounganisha vifaa vya mawasiliano.

Hali hiyo pia imeleta ushindani kwenye elimu, kutokana na ukweli kwamba, TEHAMA inampa mwanafunzi maarifa zaidi ya kupata taarifa, ujuzi na elimu kupitia vyombo vya mawasiliano, kama simu na kompyuta.

Kutokana na umuhimu huo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeanzisha somo la TEHAMA kwa elimu ya msingi na sekondari ili kuwawezesha Watanzania kujiona kuwa ni sehemu ya dunia ambayo sasa ni kijiji kimoja.

Baadhi ya wadau wa elimu nao wanaendesha kampeni na mafunzo ya kuwahamasisha wasichana kupenda masomo ya sayansi, kuwa wabunifu na kupenda kujifunza TEHAMA.

Pamoja na juhudi hizo, kumekuwapo na changamoto ambazo ni vyema zingefanyiwa kazi ili somo hilo liweze kufundishwa kwa ufasaha na pia lienee katika shule za umma nchini.

Miongoni mwa changamoto hizo, ni baadhi ya walimu kukosa mafunzo ya somo hilo na pia shule nyingine kutokuwa na umeme hali ambayo inaleta ugumu kwa walimu na wanafunzi kufundisha au kujifunza TEHAMA.

Baadhi ya walimu wa shule za vijijini, wanadai kwamba wametengwa, kwa madai kwamba, hawapati mafunzo kuhusu TEHAMA, na hata wakiyapata, hawawezi kuyatumia kwa kuwa shule zao hazina umeme.

Katika mazingira hayo, wanasema, wanalazimika kufundisha wanafunzi kwa nadharia badala ya vitendo, hali ambayo inawafanya wabaki nyuma kwenye eneo hilo.

Wanatamani wanafunzi wa shule za vijijini wajifunze TEHAMA kwa vitendo ili nao wawe na ubora kama walivyo wenzao wanaosoma mijini.

Kimsingi, madai hayo ya walimu yanaweza kuwa na uzito na ingefaa kama yangefanyiwa kazi, ili kuwaongezea uelewa wa somo hilo badala ya kuwachorea kompyuta kwenye ubao.

Kuwachorea kompyuta ubaoni, ni, wanaweza kuelewa, lakini huenda hatua hiyo haiwasaidii mwanafunzi kuelewa kifaa hicho kikamilifu.

Umeme utafanikisha somo hilo kufundishwa kwa vitendo katika shule zote na mafunzo ya walimu wanaoandaliwa kufundisha TEHAMA yakawa na tija.

Hivi karibuni, Wizara ya Nishati ilitangaza kushusha gharama za kuingiza umeme majumbani hadi kufikia Sh. 27,000, hivyo nafasi hiyo ingefaa kutumika kuhakikisha kila shule zinakuwa na umeme.

Kamati na bodi ambazo shule zao hazina nishati hiyo, zingeangalia uwezekano wa kuhakikisha zinaweka mikakati ya kupata umeme, ili kufanikisha somo hilo kwa wanafunzi wote wa mijini na vijijini.

Unafuu wa gharama za umeme ungetumiwa kuhakikisha nishati hiyo inakwenda hadi vijijini, kwani huko nako wapo wanafunzi wanaohitaji kujifunza somo la TEHAMA kwa vitendo.

Ni kweli kama wanavyokaririwa na vyombo vya habari baadhi ya walimu wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wakisema inawawia vigumu kufundisha mada za TEHAMA kwa kuwa hawajawahi kutumia kompyuta.

Lakini, inaaminisha kwamba, kuwapo kwa umeme katika shule za vijijini, ni hatua ya kwanza, aidha pia suala la kila shule kuwa na kompyuta ni la pili, hivyo ingefaa mikakati kuwapo kwa nishati hiyo kupewa mkazo.

# Samia mgeni rasmi Siku ya Ukimwi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, ambayo kitaifa yatafanyika Desemba Mosi mwaka huu jijini Mbeya.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maadhimisho hayo, ambapo alisema yatazinduliwa rasmi Novemba 24, mwaka huu.

Alisema maadhimisho hayo yataanza kwa kufanya matembezi ya hisani ambayo yataongozwa na Naibu Spika, Dk. Tulia Akson na kwamba lengo la matembezi hayo itakuwa kukusanya fedha kwa ajili ya kutunisha mfuko wa mapambano dhidi ya Ukimwi.

Homera alisema matembezi hayo yataanzia katika Kituo cha daladala cha Kabwe jijini Mbeya mpaka katika Uwanja wa CCM Ruanda Nzovwe, ambapo ndipo maadhimisho hayo yatafanyika na kwamba katika matembezi hayo zimeandaliwa fulana maalumu ambazo washiriki watazinunua.

Vilevile, alisema matembezi hayo yatafuatiwa na mdahalo wa wanafunzi wa vyuo vikuu na vyuo vya kati vilivyopo mkoani Mbeya pamoja na majadiliano ya viongozi wa dini na mila kuhusu namna ya kukabiliana na Ukimwi.

"Siku ya kilele ambayo itakuwa ni Desemba Mosi tunategemea mgeni rasmi awe Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan na ameshathibisha kuwa atakuwapo, hivyo nawasihi wananchi wa Mkoa wa Mbeya na wa mikoa jirani wajitokeze kwa wingi," alisema Homera.

Homera alisema siku moja kabla ya maadhimisho hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Bunge, Vijana na watu wenye ulemavu, Jenista Mhagama atafunga kijiji cha vijana.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alisema maandalizi kwa ajili ya maadhimisho hayo yamekamilika na kwamba wamealika wadau na taasisi mbalimbali ambao wamethibitisha kuwa watashiriki.

Alisema wakati wa maadhimisho hayo huduma mbalimbali za kiafya zitakuwa zikitolewa kwa wananchi ikiwemo upimaji wa magonjwa mbalimbali ikiwamo kifua kikuu.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (NACOPHA), Joceline Mtono, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jukwaa la wanawake wanaoishi na VVU nchini alisema watayatumia maadhimisho hayo kuwahamasisha wananchi kupima afya zao.

# Majaliwa ahadharisha matumizi fedha za ujenzi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini ikiwamo Wilaya ya Ruangwa na kuagiza fedha hizo zitumike kama ilivyokusudiwa.

Pia ameagiza wenyeviti wote wa kamati za ujenzi wa miradi hiyo ikiwamo ya ujenzi wa vituo vya afya pamoja na shule watoke katika vijiji ambavyo miradi husika inatekelezwa ili kurahisisha usimamizi.

Alitoa agizo hilo jana wakati akikagua ujenzi wa Shule ya Sekondari Kitandi, Kata ya Likunja wilayani Ruangwa, Lindi akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua shughuli za maendeleo mkoani humo.

Aliwataka watu wote walioko kwenye kamati zinazosimamia miradi hiyo wawe waadilifu na wahakikishe wanadhibiti vitendo vya wizi katika maeneo yote yanayotekelezwa miradi na ijengwe kwa viwango. "Lazima tuzilinde fedha zilizotolewa na Rais wetu mpendwa."

Vile vile, alisema mpango wa Rais Samia ni kuhakikisha Watanzania wanapata huduma zote za kijamii ikiwamo afya, maji, umeme, barabara ili kuwarahisishia kutekeleza shughuli zao. "Maendeleo haya yote ni kutokana na juhudi za mkuu wa nchi, lazima tumuunge mkono."

"Kiongozi wa nchi ametoa fedha, hatuwezi kuvumilia kuona mtu mzembe kwenye miradi ya serikali, huu ni ujumbe kwa kamati zote zinazosimamia ujenzi wa miradi nchini. Wananchi wanatajaria kuona miradi hii inakamilika, simamieni miradi na iishe tena kwa viwango, Mheshimiwa Rais Samia anatoa fedha kwa ajili ya miradi hii ya wananchi."

Aliwataka wajumbe wote wa kamati za ujenzi wa miradi nchini washirikishwe kwenye hatua zote za ujenzi ikiwamo ununuzi wa vifaa vya ujenzi.

Kwa upande wake, Katibu wa Mradi huo, Mwalimu Arafa Msuya, alisema ujenzi wa shule hiyo mpya ya sekondari ya Kitandi ambayo ni ya bweni itakayosajili watoto wa kike na kiume kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita itapunguza adha ya wanafunzi wa maeneo hayo kutembea umbali mrefu hadi Shule ya Sekondari ya Likunja.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imepokea Shilingi bilioni moja kutoka Serikali Kuu kupitia mradi wa EP4R kwa ajili ya ujenzi wa shule huo unaojumuisha miundombinu ya majengo 16 ambayo ni jengo la utawala, majengo matano yenye jumla ya vyumba 13 vya madarasa.

Miundombinu mingine ni ujenzi wa mabweni manne yakiwamo mawili ya wanafunzi wa kike na mawili ya wanafunzi wa kiume, nyumba mbili za walimu kila mmoja yenye uwezo wa kuishi familia mbili, bwalo la chakula na jiko la nje, matundu 30 ya vyoo na ujenzi wa kichomea taka.

Kwa upande wao, mafundi wanaojenga mradi huo kupitia mfumo wa force account wameishukuru serikali kwa kutoa fedha za ujenzi wa mradi huo ambao pia unatoa ajira kwa wananchi wengi hususani wanaoishi katika maeneo ya karibu.

**IMETOLEWA NA:**
**OFISI YA WAZIRI MKUU,**
**JUMATATU, NOVEMBA 22, 2021**




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (katikati), akiwa pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu Mines and Fertilizers Ltd, Pardeep Singh Hans (watatu kushoto), Kaimu Mkurugenzi wa Mikopo na Biashara TADB, Afia Sigge (watatu kulia), Meneja Mkuu wa Minjingu Mines and Fertilizers, Anup Modha (wapili kushoto), Katibu Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji TADB, Colleta Ndunguru (kushoto), Meneja wa Kanda ya Kati wa TADB, Yodas Mwanakatwe (wapili kulia), na Meneja wa Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo, Asha Tarimo (kulia), wakati benki hiyo ilipotembelea makao makuu ya ofisi ya kiwanda hicho cha mbolea mjini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EU yaunganisha nguvu kupinga ukatili

**Na Salome Kitomari**

NCHI za Umoja wa Ulaya (EU) zimeunganisha nguvu katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia nchini.

Katika kampeni ya siku 16, nchi hizo kwa kushirikiana na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UN Women na UNFPA, walipongeza jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kupambana na ukatili wa kijinsia ambao ni ukatili wa haki za binadamu.

Mabalozi hao walitoa tamko la pamoja mbele ya waandishi wa habari Dar es Salaam, kuunga mkono jitihada za kupambana na ukatili wa kijinsia kupitia kukemea na kufadhili miradi mbalimbali ya kuijengea uwezo jamii.

Viongozi hao ni Mkuu wa Ujumbe wa Umoja wa EU, Manfredo Fanti; aliyeambatana na mabalozi na nchi zao kwenye mabano ambao ni Nabil Hajlaoui (Ufaransa), Mary O'Neil (Ireland), Mette Norgaard Dissing-Spandet (Denmark), Naibu Balozi Job Runhaar (Uholanzi), Dk. Katrin Bornemann (Mkuu wa ushirikiano Ujerumani), Jacqueline Mahon (Mwakilishi wa UNFPA) na Hodan Adou (Mwakilishi wa UN Women Tanzania).

Fanti alisema kampeni ya siku 16 inalenga kuongeza uelewa kuhusu matokeo ya ukatili kwa wanawake na wasichana wadogo ambayo itaanza Novemba 25, ikiwa ni siku ya kimataifa ya kuondoa ukatili dhidi ya wanawake na kilele ni Desemba 10 ambayo ni siku ya haki za binadamu.

Balozi wa Ufaransa nchini, Hajlaoui alisema kampeni hiyo inafafanua kuwa ukatili wa kijinsia kwa wanawake ni ukatili wa haki za binadamu na kwamba wanawake, wasichana, wanaume na wavulana ni lazima kusimama pamoja kupinga ukatili.

"Ufaransa itaendelea kupinga ukatili wa kijinsia ikiwa ni kuhamasisha uwakilishi wa kutosha wa wanawake. Tumeendelea kufadhili miradi mbalimbali ya kuwajengea uwezo wanawake na wasichana ambayo imeleta matokeo makubwa,"alisema.

Fanti alisema mabalozi hao kwa kushirikiana na UN Women na UNFPA wanafanya maadhimisho hayo chini ya kauli mbiu ya "Ewe mwananchi. Komesha ukatili wa kijinsia sasa."

Balozi wa Denmark nchini, Norgaard alisema kila mwana jamii ana nafasi ya kubadili mtazamo na kukomesha matukio ya ukatili kwa kuwa vinaonekana kama vitendo vya aibu kiasi cha watendewa kushindwa kutoa taarifa.

Naye, Mwakilishi wa Balozi wa Ujerumani, Bornemann, alisema nchi hiyo inapongeza jitihada za Tanzania kwa juhudi zake katika kupambana dhidi ya ukatili wa kijinsia na kwamba katika mkutano wa 39 wa mapitio ya haki za binadamu yaliyofanyika Geneva Novemba 5,mwaka huu, ilipongezwa kwa kuandaa mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mwakilishi wa UNFPA, Mahon alisema ukatili wa kijinsia ni kikwazo kikubwa kwa wanaotendewa kwa kuwa wanakosa haki ya elimu, kuishi na kufurahia maisha kama watu wengine.

Naye, Mwakilishi wa UN Women, Adou alisema mapambano hayo yanahitaji ushiriki wa wadau wote katika kuhakikisha wanawake na watoto wanafurahia maisha kama wengine.

Katika kampeni hiyo kutakuwa na shughuli mbalimbali zitakazofanywa na balozi hizo ikiwamo kampeni mtandaoni, siku ya kimataifa ya wenye ulemavu, usalama mtandaoni, umuhimu wa utafiti katika kupambana na ukatili wa kijinsia, mkutano wa kikanda kujadili ukatili , Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu na kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuandika habari hizo kwa wingi.

# Serikali yaombwa kuunganisha sera ya viwanda, elimu sasa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Prof. Eliamani Sedoyeka, amesema ni wakati mwafaka kwa serikali kuziunganisha sera ya viwanda na ya elimu, ikiwa ni pamoja na kuanzisha shule za sekondari za ufundi kila tarafa na wilaya vyuo vya stashahada ya ufundi.

Hayo aliyasema jana mbele ya Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Samia Suluhu Hassan, alipokuwa katika hafla ya kutunuku maofisa 61 wa kundi la pili wa Shahada ya kwanza ya Sayansi ya Kijeshi inayotolewa Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli (TMA) kwa kushirikiana na Chuo cha IAA tawi la Arusha, mkoani hapa.

Alisema uwapo wa vyuo hivyo utawajengea vijana ujuzi na maarifa ya kuunda bidhaa mbalimbali, kujiajiri na kuajiri wenzao pamoja na kuunda viwanda vidogo ambavyo vitakua na kufikia vya kati na vikubwa.

"Kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia, ni wakati muafaka kwa serikali kuanzisha vyuo hivi ili kuwavutia wawekezaji wa nje na ndani ya nchi kutokana na upatikanaji wa rasilimali watu wenye ujuzi na maarifa," alisema.

Prof. Sedoyeka alisema chuo kipo tayari kushirikiana na ofisi za wakuu wa mikoa na wilaya kwa kutumia uzoefu walionao chuoni hapo pamoja na vyuo vingine ili vianzishwe.

Alisema ongezeko la vijana wanaohitimu darasa la saba na kidato cha nne ni kubwa kutokana na serikali kuendelea kutoa elimu bure na kila mwezi inatoa Sh. bilioni 24.

"Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu ulishawahi kutoa maelekezo ya mabadiliko kwenye mitaala yetu ili kuendana na mahitaji ya sasa na dira ya taifa inayolenga kwenye Tanzania ya viwanda, hivyo naomba maelekezo hayo yafanyiwe kazi ili tuweze kuwa na shule na vyuo hivyo vya ufundi ngazi ya tarafa na wilaya," alisema.

Kuhusu chuo hicho ambacho kinatoa mafunzo ya kozi mbalimbali kufanya utafiti na kutoa ushauri unaoendana na taaluma zinazotolewa chuoni hapo, wamefanikiwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kwa miaka saba na umeanza kuzaa matunda.

Alisema IAA kwa sasa ina matawi matatu likiwamo la Dar es Salaam, Manyara na Arusha na kwa sasa wapo kwenye utaratibu wa kufungua tawi lingine Dodoma.

"Chuo hiki kwa sasa kinatoa kozi zaidi ya 60 katika ngazi ya cheti, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili na tutaansa kutoa Shahada ya Uzamivu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Nelson Mandela Januari mwakani," alisema.

Licha ya mafanikio hayo Prof. Sedoyeka alisema, chuo hicho kinakabiliwa na changamoto ya wakufunzi na wafanyakazi kutokana na sekta hiyo kutoajiri wakufunzi wa vyuo mbalimbali nchini kwa miaka sita.



Marais wa Vyama vya Wafanyabiashara Tanzania (TCCIA) na India, Paul Koyi (watatu kushoto) na Atul Kumar Saxena (IICIA), wakionyesha hati za makubaliano waliyotia saini katika ofisi za TCCIA jijini Dar es Salaam, hivi karibuni. Wanaoshuhudia; Anisa Mbega ambaye ni Balozi Mteule wa Tanzania nchini India na Kaimu Balozi wa India nchini Tanzania, Raj Ganger. **PICHA: UBALOZI WA INDIA**

# Mgombea Demokrasia Makini aahidi mambo kibao Ngorongoro

**Na Thobias Mwanakatwe,** NGORONGORO

MGOMBEA ubunge katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Ngorongoro mkoani Arusha kupitia Chama cha Demokrasia Makini, Simon Ngilisho, amesema iwapo atapata ridhaa ya wananchi atahakikisha kinajengwa kiwanda cha ngozi.

Aidha, amesema fedha zote za mfuko wa jimbo zitakazotolewa zitaelekezwa katika kuwasomesha watoto yatima na ambao wazazi wao hawana uwezo ili kuinua kiwango cha elimu katika jimbo hilo.

Ngilisho alisema hayo kwa nyakati tofauti katika mikutano yake ya kampeni aliyoifanya katika kata za Waso, Engarasosabo, Samunge, Osinoni na Olipilo na kuwaahidi wananchi mambo mbalimbali iwapo watamchagua kuwa mbunge wao.

Alisema kwa kuwa asilimia 70 ya wananchi wa Jimbo la Ngorongoro ni wafugaji, hivyo ili waweze kunufaika na ufugaji ni kuwajengea kiwanda cha ngozi, ambacho kitatengeneza bidhaa kama viatu, mikoba ya kinamama na nyingine mbalimbali.

Aliongeza kuwa jambo jingine atakalolifanyia kazi ni kuhakikisha zinajengwa shule za kutosha za awali, msingi na sekondari ili kutoa fursa kwa watoto wengi wa wafugaji kupata fursa ya kusoma.

"Jimbo hili wafugaji ni wengi kwa hiyo unakuta watoto hawapati fursa ya kusoma na badala yake wanachunga mifugo tu... hali hii inachangiwa na kuwa na shule chache, lakini iwapo zitajengwa shule nyingi tatizo la kutaka watoto wakachunge halitakuwapo bali watapelekwa shule," alisema.

# Rais Mwinyi akutana na kiongozi Kanisa la Efatha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amepongeza utayari wa uongozi wa Kanisa la Efatha wa kuunga mkono juhudi za Serikali ya Zanzibar kuleta maendeleo pamoja na kuimarisha huduma za kijamii.

Rais Dk. Mwinyi alitoa pongezi hizo jana wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na uongozi wa Kanisa la Efatha lenye Makao Makuu yake Mwenge, jijini Dar es Salaam, ukiongozwa na Kiongozi Mkuu wa Kanisa hilo, Josephat Elias Mwingira, Ikulu, kwa ajili ya kumpongeza Rais.

Rais Dk. Mwinyi alisema anafarajika kwa kiasi kikubwa anapopata watu wa kumuunga mkono katika kuendeleza shughuli mbalimbali za maendeleo na kijamii katika kuwahudumia wananchi.

Alisema hatua za uongozi wa kanisa la Efatha zinatoa matumaini makubwa katika kuhakikisha juhudi anazozifanya zinathaminiwa na kuungwa mkono na tangu alipoingia madarakani ameshuhudia makundi kadhaa ya kijamii yakiwamo madhehebu ya kidini yakionyesha ushirikiano mkubwa kwake pamoja na serikali anayoiongoza.

Alisema mafanikio makubwa yamepatikana katika uongozi wake kutokana na wananchi kuwa wamoja na kuondokana na matabaka katika jamii yakiwamo ya kidini.

Pia, alipongeza hatua za kanisa hilo kuunga mkono juhudi za serikali katika kuimarisha sekta ya elimu, afya pamoja na ujenzi wa vituo vya polisi kusaidia kwa kiasi kikubwa katika kuleta maendeleo kwa wananchi na kutoa huduma za kijamii.

Alisema kwa vile Zanzibar ni nchi ya utalii, hatua za ujenzi wa vituo vya polisi zitasaidia kuimarisha amani na usalama kwa wananchi pamoja na wageni wanaokuja kuitembelea kwa kuamini kwamba nchi iko salama.

Kwa upande wa sekta ya elimu, Rais Dk. Mwinyi alisema, hivi sasa Zanzibar imo katika hatua za makusudi za kufanya mageuzi ya elimu na hatua za uongozi huo za kuahidi kushirikiana na serikali ikiwa ni pamoja na kuwatumia watalamu wake zitasaidia kufikia lengo hilo lililokusudiwa.

Rais Dk. Mwinyi aliuahidi uongozi huo kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari na itaendelea kuweka mazingira mazuri kuhakikisha azma inapatikana.

Naye Kiongozi Mkuu wa Kanisa hilo, Mwingira, alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kupata neema ya kuwa Rais wa Zanzibar na ndani ya mwaka mmoja mafanikio makubwa yamepatikana.

Mwingira alisema Rais Mwinyi ana hofu ya Mungu na ameweza kuwaunganisha wananchi wa makundi yote bila ya kujali dini, chama, kabila wala jinsia.

Alisema utendaji wake umefanikiwa kutokana na kiongozi huyo kutokuwa na ubaguzi wa aina yoyote na kwa upande wao wakiwa viongozi wa Kanisa la Efatha, wameridhika na juhudi hizo na kuahidi kumuunga mkono yeye na serikali anayoiongoza ili mafanikio zaidi yaweze kupatikana.

# Mabinti balehe wapewa vifaa

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MABINTI balehe na kinamama vijana 30 wanaoishi katika mazingira magumu, wamefadhiliwa vifaa mbalimbali vya ufundi bure na Shirika lisilo la kiserikali la FHI360 vyenye thamani ya Sh. milioni 42, ili kutatua changamoto ya ukosefu wa mitaji.

Vifaa hivyo ni vyerehani vinane, photokopi nne, vifaa vya umeme vitatu, vifaa vya saluni vitatu, mashine za uchomeleaji saba, viti vya saluni sita, mikasi ya cherehani nne, sindano nne, majora manne, compresa sita na tape meja nne, vilitolewa na shirika hilo kwa ufadhili wa PEPFAR na USAID.

Akikabidhi vifaa hivyo, Meneja wa mradi wa Epic mkoa wa Shinyanga, Dk. Shinje Msuka katika mahafali ya 18 ya Chuo cha Ufundi Mwakata (SFS), alisema, vifaa hivyo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa kusaidia wasichana wanaoishi katika mazingira magumu wasipate maambukizi mapya ya VVU na Ukimwi.

Alisema, vifaa hivyo vitasaidia kuondoa changamoto ya ukosefu wa mitaji kwa wahitimu hao na kutoingia kwenye mikopo yenye riba kubwa ambayo inawafanya kushindwa kukua kwenye shughuli zao.

# Zawadi za mil. 73/- sasa zatolewa NMB Bonge la Mpango

**Na Mwandishi Wetu**

KIASI cha Sh. milioni 73 kimetolewa msimu wa pili wa kampeni ya Weka Akiba na Ushinde inayoendeshwa na Benki ya NMB 'Bonge la Mpango - 2merudi Tena.

Fedha hizo zimetolewa katika kipindi cha wiki sita, kati ya Sh. milioni 237 zinazoshindaniwa.

Kampeni hiyo ni ya miezi mitatu (Oktoba hadi Desemba 2021), inayolenga kuhamasisha utamaduni wa kufungua akaunti na kuweka akiba, ambako kila wiki washindi 12 huzawadiwa, 10 walishinda pesa na wengine wawili wakitwaa pikipiki za mizigo za miguu mitatu aina ya Skymark zenye thamani ya Sh. milioni 4.5 kila moja.

Droo ya sita ya kampeni hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, ambapo Alexander Msombe wa Mwanjelwa, mkoani Mbeya na Mwanaharusi Anafi wa Dodoma, walijinyakulia pikipiki, huku washindi wengine 10 wakijitwalia pesa taslimu Sh. milioni moja kila mmoja.

Kwa mujibu wa Meneja Uhusiano Amana za Wateja wa NMB, Monica Job, tangu kuanza kwa msimu wa pili wa NMB Bonge la Mpango, thamani ya jumla ya zawadi za pesa na pikipiki zilizotolewa ni Sh. milioni 73.5, ambako washindi 60 wameshinda pesa na wengine 15 wakitwaa pikipiki.

"Kampeni kwa ujumla itatoa pikipiki 50 kwa wateja, ambako kila wiki tutatoa washindi wawili na washindi wa mwezi watatu. Kufikia leo tumetoa pikipiki 12 za kila wiki na tatu za mwisho wa mwezi wa kwanza wa kampeni hii. Pia kwa wiki sita tumetoa Sh. milioni 6 kwa washindi 60 (10 kwa kila wiki)," alisema Monica.Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Msasani, Kelvin Mwangosi, aliwataka wateja wa benki hiyo kuendelea kuweka akiba ili kujishindia zawadi mbalimbali, huku akiwakaribisha matawini Watanzania wasio na akaunti kufungua na kuweka akiba isiyopungua Sh. 100,000 ili kukidhi vigezo vya ushiriki.

# Nyumba zinazohamishika sasa kujengwa nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Kitanzania SPH Co Ltd, imesaini mkataba wa ushirikiano na kampuni ya kimataifa ya ujenzi ya Al Masaood Bergum yenye makao yake makuu Abu Dhabi, Falme za Kiarabu.

Mkataba huo wa ushirikiano, utaziwezesha kampuni hizo mbili kufanya kazi pamoja katika miradi ya ujenzi wa nyumba zinazohamishika nchini na hata nje ya mipaka ya nchi.

Mkataba huo ulisainiwa wakati wa Maonyesho ya Kimataifa ya Petroli ya Abu Dhabi (ADIPEC) kati ya Mkurugenzi Mtendaji wa SPH, Salim Mbarouk Salim na mkuu wa masuala ya biashara wa kampuni ya Al-Masaood, Hani El Tannir. Pamoja na mambo mengine, mkataba huo utaziwezesha kampuni hizo mbili kufanya kazi kuanzia hatua za mwanzo za utekelezaji wa miradi mpaka kumalizika kwake.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, Mkurugenzi wa SPH, Salim Mbarouk, alisema kampuni yake imefurahia kuingia mkataba na kampuni hiyo kubwa duniani, ambayo italeta uzoefu na maarifa mapya katika soko la ndani.

"Al- Masaood ni kampuni kubwa na ina uzoefu wa zaidi ya miaka 40 katika masuala ya ujenzi wa nyumba zinazohamishika. Katika miaka ya hivi karibuni kampuni hii imekuwa ikionyesha nia ya kufanya kazi katika masoko ya Afrika na tayari ipo nchini Algeria. SPH kama kampuni ya kizawa inaona fursa nyingi ya kufanya kazi na kampuni hii kubwa," alisema.

Mkurugenzi huyo wa SPH alisema Tanzania kwa sasa inatoa mazingira mazuri ya uwekezaji, na kwamba kampuni yake ipo tayari kufanya kazi na makampuni mbali mbali ili kunufaika na fursa zilizopo.

Aliongeza kuwa kwa kufanya kazi na kampuni kubwa na zenye uzoefu wa miaka mingi, Tanzania itaweza kupata ujuzi na maarifa mapya, lakini kupata nafasi ya kushindana katika dunia iliyotawaliwa na ushindani unaoongozwa na teknolojia mpya na za kisasa.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kitanzania ya SPH Co Ltd, Salim Mbarouk Salim (kushoto), akiwa pamoja na Hani El Tannir ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara aliyeiwakilisha Kampuni ya Al Masaood Bergum WLL ya Falme za Kiarabu wakitia saini mkataba wa ushirikiano wa kampuni hizo, baada ya kumalizika kwa maonyesho ya kimataifa ya mafuta na gesi ya Abu Dhabi (ADIPEC). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC alivyokerwa mimba za wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, ameagiza wakuu wa wilaya za mkoa huo kuhakikisha wanafuatilia na kudhibiti kuongezeka kwa wanafunzi wa kike wanaokatisha masomo kutokana na mimba.

Akizungumza mjini Sumbawanga, Mkuu huyo wa Mkoa alionyesha kutofurahishwa na kasi ya kuongezeka kwa wanafunzi wa kike wanaoshindwa kukamilisha masomo yao sababu ikitajwa kuwa ni kupata ujauzito.

"Lazima tuongeze mapambano kudhibiti mimba za utotoni. Sijafurahishwa kuona Wilaya ya Nkasi ikiwa na idadi ya wanafunzi 25 mwaka huu waliopata mimba wakiwa wanasoma. Hii haikubaliki. Wakuu wa wilaya nendeni mkadhibiti vitendo hivi," alisisitiza Mkirikiti.

Takwimu za Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Rukwa zimeonyesha kuwa katika mwaka huu 2021 Wilaya ya Nkasi imekuwa na matukio 25 ya wanafunzi wa kike kupata mimba huku Wilaya ya Kalambo ikiripoti wasichana wanane na Wilaya ya Sumbawanga nayo ikiwa na wanafunzi wanane.

Mkirikiti aliagiza pia Maofisa Elimu Kata kutimiza majukumu yao kwa kufuatilia walimu na watu wanaojihusisha na kuwapatia mimba wanafunzi kwani zipo taarifa baadhi ya walimu wanahusika na vitendo hivyo kinyume na maadili ya kazi.

"Maofisa Elimu Kata mmepewa pikipiki na serikali ili zitumike kutekeleza majukumu ya kusimamia elimu kwenye shule ikiwamo kufuatilia wazazi na walezi wasiolea watoto wao hatua inayosababisha baadhi ya watoto wa kike kupata mimba na watoto wengine kuacha shule bila sababu," alisitiza Mkirikiti.

Aidha, Mkirikiti amemwagiza Ofisa Elimu Mkoa wa Rukwa, Samson Hango, kuhakikisha timu anayoiongoza inajipanga kuchukua hatua kali za kinidhamu na kisheria kwa walimu wote wanaoshabikia mimba za utotoni kwenye maeneo yao.

Katika hatua nyingine Mkirikiti ameagiza vijana wa skauti kote mkoani Rukwa kutumika na halmashauri kubaini wazazi wanaotekelekeza watoto na kusababisha wahamie mitaani na kuitwa 'watoto wa mtaani' ambao wanazidi kuongezeka hususan Manispaa ya Sumbawanga.

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Sebastian Waryuba, alisema atahakikisha anashirikiana na vijana hususan skauti kufundisha vijana umuhimu wa maadili mema ili waweze kuwa raia wema na kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi.

# Wanavijiji walia kutumia maji ya madimbwi

**Na Lilian Lugakingira,**
MISSENYI

WAKAZI wa vijiji vitatu vya Kata ya Kakunyu Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, wanalazimika kutumia maji ya madimbwi na tingatinga kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kutokana na vijiji hivyo kutokuwa na maji ya bomba.

Wakizungumzia kadhia hiyo, wakazi hao wa vijiji vya Bwenkoma, Bugango na Kakunyu walisema wanatumia maji hayo kwa muda mrefu ambayo siyo salama kwa afya zao na kuomba serikali kuwafikishia maji ya bomba.

"Lakini wakati wa msimu wa kiangazi madimbwi haya hukauka, hali hii hutufanya kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 17 kufuata maji nchi jirani ya Uganda, maana vijiji vyetu vipo mpakani," alisema Bosco Kashunju, mkazi wa kijiji cha Bwenkoma.

Alisema kuwa tangu uwepo wa ugonjwa wa UVIKO-19 wamesitisha kwenda nchini Uganda kufuata maji, na kwamba sasa wanahofia zaidi usalama wa afya zao kutokana na maji ya madimbi na tingatinga wanayotumia kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

Naye Jovitha Meshack, mkazi wa kijiji cha Bugango aliiomba serikali kuwasaidia kupata maji ya bomba ili kuwaondolea tatizo hilo ambalo linahatarisha afya zao, huku akidai kuwa wanaoteseka zaidi kufuata maji ni wanawake na watoto.

"Ili kuwaondolea wananchi hao adha hiyo, mwaka 2014 serikali ilianza ujenzi wa mradi wa maji katika vijiji hivyo uliokamilika mwaka 2018 kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 875, lakini mpaka sasa mradi huo umeshindwa kutoa matumaini kwa wananchi kutokana na mashine ya kusukuma maji kukosa mafuta," alisema.

Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RUWASA), Andrew Kilembe, alikiri vijiji hivyo kuwa na adha hiyo, lakini akasema wanafanya kila jitihada kuhakikisha adha hiyo inakwisha na wananchi wanapata majisafi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

"Tunaendelea na mazungumzo na Shirika la Umeme (TANESCO), ili wafunge umeme katika eneo ulipojenga mradi huo, lengo likiwa ni kuhakikisha mashine ya kusukuma maji inafanya kazi muda wote na wananchi wanapata maji ya kutosha," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga (kushoto), akikabidhi zawadi ya pampu ya kupulizia dawa mikorosho kwa mmoja wa washindi wa droo ya tatu ya kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani' inayoendeshwa na Benki ya NBC mahususi kwa wakulima wa korosho mikoa ya Lindi na Mtwara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC: Wakulima wa korosho jiwekeeni akiba

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, amewashauri wakulima wa korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara kujiwekea akiba sambamba na kufungua akaunti za akiba kwa ajili ya watoto.

Amesema kwa kufanya hivyo itawasaidia kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha ili kujikwamua na umaskini.

Akizungumza mwishoni mwa wiki mkoani humo wakati wa kukabidhi ya zawadi mbalimbali kwa wakulima wa korosho mkoa wa Mtwara walioibuka washindi wa droo ya tatu ya kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani', Ndemanga alisema licha ya wakazi wa mikoa hiyo kupata fedha nyingi kupitia kilimo cha mazao ya korosho na ufuta, bado wamekuwa na changamoto za kifedha hususani katika masuala muhimu ikiwamo ada za watoto kutokana na ukata mkubwa unaotokana na wao kutojiwekea akiba.

"Kwa kuwa muda ambao tunapata fedha zitokanazo na kilimo huwa hauendani na muda wa kulipa ada za watoto wetu kumekuwa na ufujaji mkubwa wa fedha kwa matumizi yasiyo na tija sana. Ni kutokana na changamoto hiyo ndio sababu nawaomba sana mjenge utamaduni wa kujiwekea akiba ili isaidie muda sahihi ukifika," alisema.

Aliwashauri wakulima hao kufungua akaunti hizo kupitia benki ya NBC kutokana na ukaribu uliopo kati ya wakulima hao na benki hiyo, huku akitolea mfano wa akaunti ya NBC Shambani iliyobuniwa mahusussi kwa ajili ya wakulima.

"Kwa kuwa jitihada hizi za NBC zimeonyesha kuunga mkono juhudi za wakulima na serikali katika kuboresha kilimo cha korosho katika mikoa ya Mtwara na Lindi ni vema pia tuendeleze ushirikiano huu pia hata kwenye akaunti nyingine zikiwamo za akiba na watoto wetu ili kuimarisha zaidi uhusiano wetu na zaidi tukiamini kwamba akufaaye kwa dhiki ndio rafiki wa kweli," aliongeza.

Aidha, aliwataka wakulima hao kutumia ipasavyo zawadi mbalimbali walizozipata wakulima hao kupitia kampeni hiyo ikiwamo pikipiki, baiskeli, pampu za kupulizia dawa mikorosho ili viweze kuwasaidia katika kujiongezea uzalishaji wa mazao yao sambamba na kujiandaa vema kwa ajili ya msimu ujao.

Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Kusini, Zubeider Haroun, alisema kupitia droo hiyo ya pili benki ilitoa zawadi za aina mbalimbali ikiwamo pikipiki, baiskeli, pampu za kupulizia dawa mikorosho, guta (Toyo), pamoja na zawadi za nyingine ikiwamo kanga, mabegi ya shule na madaftari kwa wakulima mmoja mmoja na AMCOS katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

"Kampeni hii inalenga kusaidia jitihada zilizowekwa na serikali za kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 280,000 zinazozalishwa sasa hadi kufikia tani 700,000 ifikapo mwaka 2025 sambamba na kuwahamasisha wakulima wa korosho kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza uzalishaji."

Washindi wa droo hiyo walishukuru benki ya NBC kwa kuandaa kampeni hiyo kwa kuwa imekuwa na msaada mkubwa kwao.

# Wateja mafuta wapewa fursa kutoa maoni

**Na Christina Mwakangale**

KAMPUNI ya TotalEnergies Marketing Tanzania, imezindua awamu ya tatu ya wiki ya huduma kwa wateja, kwa kuwapa fursa ya kusikiliza maoni yao, ili kuboresha mahusiano na huduma.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Jean-Francois Schoepp, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, alisema ushirikishwaji wa wananchi kwenye kila huduma wanayoipokea inaleta maboresho na kukuza biashara.

"Kama Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kusema kuwa, ikiwa maendeleo ya kweli yatatokea, ni lazima wananchi washirikishwe. Pia tunaamini kwamba TotalEnergies Marketing Tanzania Limited, itaendelea kukua zaidi endapo tutawashirikisha wateja wetu kukidhi mahitaji kikamilifu," alisema Schoepp.


Alisema, kampuni hiyo katika awamu hii ya tatu ya huduma kwa mteja tangu, ianzishwe mwaka 2019, inaendelea kuonyesha dhamira yake kwa Watanzania kwa kuwakaribisha wateja wao, kushiriki maono yao ya mustakabali wa kampuni hiyo nchini.

Awali, wafanyakazi wa kampuni hiyo, wakiongozwa na Schoepp, walitoa huduma kwa wateja waliofika kwenye kituo cha TotalEnergies East Oysterbay, kwa kusikiliza maoni ya wateja, ili kuboresha mahusiano na wateja wao.

Kadhalika, wateja walipata nafasi ya kucheza gurudumu la bahati katika kituo hicho na kujishindia zawadi kadhaa zikiwamo fulana, chupa za maji, kofia, bidhaa za kutunza magari kama vile air freshener na vocha inayowawezesha kununua bidhaa zozote katika duka la Cafe Bonjour, liliopo kituoni hapo.


"TotalEnergies Marketing Tanzania Limited, imekuja na taswira mpya na kuwa wabunifu zaidi, hii inaakisiwa kikamilifu na ushirikishwaji wa wateja wao kwa nia ya kuboresha ubora wa bidhaa na huduma zao, ili kukidhi haja ya kila Mtanzania anayehitaji huduma za mafuta, vilainishi," alisema mkurugenzi huyo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 23, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

## ‘Vijiji vinapoamua kujijengea Chuo cha VETA’



Ukurasa 12

## Ukweli sayari mpya kujulikana

ELIMU

NA FAUSTINE FELICIANE

# HATARI JUA KALI USICHUKULIE POA

- Ni chanzo kupoteza maji, kuathiri ubungo, figo



Kuponda kokoto ni kazi inayofanyika wakati mwingi juani, msimu huu wa jua kali ni vyema kuchukua tahadhari. **PICHA: MTANDAO**

MWAKA huu mabadiliko ya tabianchi yamekuwa bayana au dhahiri kila sehemu kwa sababu karibu mikoa yote nchini inazungumzia kuongezeka kwa joto na uhaba wa mvua.

Kila mahali mijini na vijijini watu wanalalamikia ongezeko la joto pamoja na ukame na eneo la West Kilimanjaro kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), ndiyo sehemu yenye joto kubwa linalofikia nyuzi 36.

TMA inaeleza ongezeko la joto kwenye mikoa mingi mwaka huu, hali isiyokuwa ya kawaida wakati Kilimanjaro jua ni kali na joto limeongezeka na kufika nyuzi 36 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya nyuzi 3.5 ikilinganishwa na miaka ya nyuma, hivyo kuweka rekodi mpya kwa mkoa huo unaosifika kuwa na hali ya hewa ya baridi ikilinganishwa na maeneo mengine ya Tanzania.

Joto ni kali bara na visiwani Zanzibar likipaa kuelekea zaidi ya nyuzi 35, hivyo kutokana na hali hiyo wananchi wanakumbushwa kuzingatia masuala muhimu katika kipindi hiki.

Meneja wa kituo kikuu cha utabiri cha TMA, Samuel Mbuya, anasema hali ya joto imekuwa kubwa hapa nchini kutokana na sababu kuu mbili ya kwanza ikiwa ni upungufu wa mvua kwenye maeneo mengi.

Lakini, sababu ya pili ni jua la utosi kwa sasa linapita katika uso wa Tanzania baada ya kuvuka mstari wa Ikweta, sababu hizo zote kwa pamoja ndizo zimepelekea hali hiyo ya joto kali, anasema Mbuya.

Anaongeza kuwa kawaida katika mwezi Novemba, joto linaongezeka kwenye mikoa ya kusini lakini kwa sasa hali ni tofauti baada ya kushuhudiwa joto kali mikoa ya kaskazini.

“Hali hii ya joto kali tunategemea itaendelea kwa kipindi chote cha Novemba na tunategemea itaanza kupungua Desemba kwa sababu tunaimani mvua zitakuwa zimeanza kutapakaa kwenye baadhi ya mikoa lakini pia jua la utosi litakuwa limeshapita katika nchi yetu,” anasema Mbuya.

Anaongeza kuwa wananchi wanapaswa kufuata maelekezo na ushauri wa wataalamu wa afya katika kukabiliana na athari zinazotokana na hali mbaya ya joto kali kiafya.

**ZINGATIA HAYA**

Daktari wa magonjwa ya binadamu kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Tawi la Mloganzila, Dk. Milagilo Malombe, anasema hali ya sasa ya joto kali lina athari kubwa kwa afya ya mwanadamu kama hakuna hatua za haraka zinazochukuliwa.

Analotaja kubwa na kuwataka watu kuzingatia ni kuupoza mwili kwa maji kwa kuoga mara kwa mara hasa maeneo yenye maji na kuepuka kukaa muda mrefu kwenye jua kali, ikiwamo kutembea juani muda mrefu bila kujifunika.

Anasema kipindi hiki mtu anapoteza maji mengi mwilini kwa njia ya kutokwa jasho jingi pamoja na njia ya mvuke.

“Lakini sio tu maji yanapungua mwilini, lakini maji hayatoki kama maji peke yake yanatoka na madini muhimu kwenye mwili wa binadamu kama ‘potashiam’”, anasema Dk. Malombe.

Anasema potashiam ikipungua mwilini husababisha ubongo kutofanya kazi yake vizuri, lakini pia kupotea kwa maji mwilini kunaathiri figo na hivyo kupelekea mtu kupata magonjwa ya figo.

“Maji yanapoingia mwilini yanakaa sehemu mbili, yanakaa kwenye seli na mengine yanakuwa nje ya seli, sasa mtu anapopoteza maji yanayoanza kutoka ni yale yaliyopo nje ya seli, yanapopungua au kuisha maji ambayo yapo ndani ya seli huanza kutoka ili kuziba nafasi, hapa sasa ndipo seli zinapokosa maji na kupelekea figo kuathirika na kushindwa kufanya kazi yake kikamilifu,” anasema Dk. Malombe.

Anataja athari nyingine za kiafya zinazotokana na kupoteza maji mengi mwilini ni pamoja na kupata magonjwa ya ngozi, lakini msongo wa mawazo.

“Maji yanapotoka mwilini kwa njia ya jasho kuna taka mwili zinabaki juu ya ngozi na watu wasipokuwa makini husababisha magonjwa ya ngozi, lakini ukosefu wa maji unampelekea mtu kuwa na msongo wa mawazo na wakati mwingine asijue sababu zake, lakini kiafya hii pia inaweza kuwa chanzo kimojawapo,”anasema Dk. Malombe.

**HATUA ZA KUCHUKUA**

Wakati TMA ikisisitiza wananchi kufuata na kutekeleza ushauri wa wataalamu, Dk. Malombe, anaeleza mambo muhimu ya kufanya katika kipindi hiki cha joto kali.

Anasema ni vyema kuoga kila wakati kila inapowezekana ili kuupoza mwili, lakini kuondoa bakteria wowote wanaokaa juu ya ngozi baada ya kutokwa na jasho.

“Pia watu wajenge mazoea ya kunywa maji, kwa kawaida tunakadiria katika kipindi kama hiki mtu anapoteza maji kwa njia mbalimbali katika kiwango cha lita tano mpaka sita kwa siku, sasa kitaalamu tunashauri angalau watu wanywe maji nusu ya yale wanayopoteza kwa maana ya kuanzia lita mbili na nusu mpaka lita tatu,” anasema Dk. Malombe.

Anashauri pia watu waepuke kukaa muda mrefu juani ili kuepusha uwezekano wa kutokwa na jasho jingi hivyo kupoteza maji zaidi na kuumia ngozi.

“Kwa wanamichezo pia wanapaswa kuchukua tahadhari katika kipindi hiki, wanapaswa kunywa maji mengi kwa sababu wakati wa mazoezi wanapoteza maji mengi zaidi,” anasema.

Anasema hali ya joto inapokuwa kubwa zaidi ya nyuzi joto 38-40 inatajwa kuwa hali mbaya zaidi ya joto inayoweza kuwaathiri watu wengi lakini ikiumiza zaidi wazee, watoto na wagonjwa.

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

# Ukweli sayari mpya kujulikana karibuni

## Roboti za China kufuata sampuli zake



Mwonekano wa sayari ya Kamo`oalewa ikiwa katikati ya mwezi na dunia. **PICHA: MTANDAO**

MIAKA ya hivi karibuni wanasayansi wamekuwa wakishangaa ni nini hasa asili ya sayari ndogo iliyopewa jina la Kamo`oalewa iliyogunduliwa mwaka 2016.

Kamo`oalewa ni jina la Kihawaii ambalo limetafsiriwa kwa Kihispania kama "kipande cha angani kinachozunguka."

Ukweli wa kukijua kimondo au sayari hiyo mpya utafahamika kutokana na juhudi za China kuunda roboti itakayokwenda mwezi kuchukua sampuli za udongo wake.

Baada ya kuonekana sayari hiyo wanasayansi walichofahamu ni kwamba iko karibu na dunia, lakini hawakuwa na taarifa zaidi kuhusu sayari ngeni.

Hata hivyo utafiti mpya na wa hivi karibuni, unaongeza jambo jipya kuhusu asili yake na inaelezwa kuwa inaweza kuwa huenda ni kipande cha mwezi na si sayari kama inavyodhaniwa.

"Haionekani kama ni ya kawaida kwa kile tulichokitarajia," anasema Benjamin Sharkey, mtaalamu wa masuala ya sayari kutoka Chuo Kikuu cha Arizona na mwandishi mkuu wa utafiti mpya uliochapishwa katika jarida la 'Nature.'

Mtafiti mwenzake wa Venezuela, Juan Sánchez, ambaye alishiriki katika uchunguzi huo, anaiambia idhaa ya Kihispaniola ya BBC Mundo: "Labda inaweza kuwa imetokea kwa sababu ya mgongano kati ya mwezi na kimondo. Inawezekana ilitoka kwenye uso wa mwezi."

Ingawa njia pekee ya kujua asili ya 'Kamo`oalewa' ni kwa kupata sampuli, jambo ambalo linaweza kutokea ndani ya muongo huu, wanasayansi wana mambo kadhaa ya kuzingatia iwapo nadharia yake ni sahihi."

> kawaida kwa kile tulichokitarajia," anasema Benjamin Sharkey, mtaalamu wa masuala ya sayari kutoka Chuo Kikuu cha Arizona na mwandishi mkuu wa utafiti mpya uliochapishwa katika jarida la 'Nature.'

### KAMO`OALEWA NI NINI?

Kamo`oalewa zamani ilijulikana kama 2016 HO3, iligunduliwa mwaka 2016 na darubini ya Pan-STARRS 1, ambayo iko Hawaii.

Wanasayansi waliipa jina la Kihawaii ambalo linaweza kutafsiriwa kwa Kihispania kama "kipande cha angani kinachozunguka."

Sayari hiyo ina urefu wa takribani mita 40 na inachukuliwa kitaalamu kama "quasi satellite", si "mwezi".

Wataalamu wanasema iko karibu na sayari dunia inapozunguka jua, Sánchez anaielezea BBC Mundo.

Mhitimu huyo wa Chuo Kikuu cha Venezuela, anasema tofauti na mwezi, Kamo`oalewa haizunguki dunia.

"Ndiyo maana ikiwa sayari yetu ingetoweka, mwamba huu ungefuata mzunguko wake wa sasa. Wanasayansi hadi sasa wamegundua sayari 'quasi-satellites' (ambazo ziko katika mtizamo wa hisia) tano zinazoweza kuitwa sayari mpya, lakini wameweza kuzungumzia taarifa za sayari hii ndogo ya Kamo`oalewa.

"Ni rahisi kuitazama hii kuliko satelaiti nyingine zinazojulikana. Mara moja kwa mwaka, wakati wa mwezi wa Aprili, kitu hiki kinang'aa vya kutosha kuweza kuangaliwa kwa darubini kubwa kutoka duniani," anasema Sánchez.

Nyingine hazionekani sana na hazikuweza kuchanganuliwa.

### MWAMBA KAMO`OALEWA

Wakati wa kuchunguza sayari hii ndogo, wanasayansi waligundua kwamba ilikuwa na rangi nyekundu isiyo ya kawaida, ishara ya kuwapo kwa madini ya metali.

"Kwa maneno rahisi, kimsingi tulichofanya ni kusoma jinsi mwanga wa jua unavyoakisiwa juu ya uso wa kitu hiki ili kujaribu kubaini kimeundwa na kitu gani. Tulichogundua ni kwamba kitu hicho kimetengenezwa kwa madini ya silicate," anasema Sánchez.

Wanasayansi hao pia walidokeza kwamba jiwe pekee linalojulikana kama mwamba ni lile la sampuli ya mwezi iliyorejeshwa kwenye misheni ya Apollo katika miaka ya 1970.

Wanasayansi wanachotaja ni kwamba hawana uhakika wa asilimia 100 na njia pekee ni kupata sampuli za sayari hiyo ili kuwa na uhakika, anasema Sánchez.

"Na kupata sampuli huenda ikawa sio jambo gumu hivyo. Ikiwa mipango ya China itaendelea vyema, muongo huu Beijing itazindua misheni ya roboti ambayo itatembelea Kamo'oalewa na kuleta sampuli."

"Kisha inaweza kuthibitishwa ikiwa Kamo'oalewa ni sehemu ya mwezi wetu tunaoujua huku duniani ama la ni kitu kingine," anaongeza mtaalamu huyo.

**BBC SWAHILI**

> "Ndiyo maana ikiwa sayari yetu ingetoweka, mwamba huu ungefuata mzunguko wake wa sasa. Wanasayansi hadi sasa wamegundua sayari 'quasi-satellites' (ambazo ziko katika mtizamo wa hisia) tano zinazoweza kuitwa sayari mpya, lakini wameweza kuzungumzia taarifa za sayari hii ndogo ya Kamo`oalewa.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA



Vifaa mfano kiti mwendo, fimbo nyeupe na vyoo rafiki vya kuhudumia wanafunzi wenye ulemavu ni mambo muhimu katika shule jumuishi. **PICHA: MTANDAO**

# Ndivyo shule inavyosaidia wenye ulemavu

## Walimu wajitoa kufundishana lugha alama

KATIKA juhudi za kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalumu, Shule ya Msingi Buhangija Jumuishi, yenye wanafunzi mchanganyiko wakiwamo wanaoishi na ulemavu imeanza kuwafundisha walimu wasio na elimu maalumu lugha ya alama ili waitumie kuwahudumia wenye ulemavu.

Walimu wenye ujuzi wa lugha ya alama wa shule hiyo iliyopo Ibinzamata katika Manispaa ya Shinyanga, huwafundisha na kuwaongezea wengine ujuzi.

Ofisa Elimu Maalum Manispaa ya Shinyanga, Edward Mdagata, anasema licha ya serikali kuanza kutatua kero zinazowakabili wanafunzi wenye ulemavu wanaosoma Buhangija, shule imeanzisha klabu ya kufundisha walimu lugha hiyo.

"Tumeanzisha klabu ya kila wiki ya kufundisha walimu wa kawaida kuzijua lugha za alama, ili wanapofundisha wanafunzi wa kawaida na wenye ulemavu kwa wakati mmoja kwenye kipindi wawe wanachanganya na lugha hizo." Anasema.

> "Nitahakikisha wanafunzi wenye ulemavu wanapata elimu sawa kama watoto wengine ambao hawana ulemavu, na pale penye changamoto nitapiga kelele sana, lengo watoto hawa watimize ndoto zao na kujitegemea katika maisha yao," anasema Sabo.

Anaongeza kuwa shule hiyo ilikuwa inakabiliwa na matatizo kadhaa hasa upungufu wa walimu na vifaa maalumu, miundombinu rafiki na kwamba matatizo hayo yameanza kutatuliwa.

Anasema licha ya kufundisha walimu lugha ya alama manispaa imeandika barua kuomba walimu wenye taaluma maalum waliko kwenye halmashauri ya wilaya ya Shinyanga wanaofanyakazi shule za kawaida, wahamishiwe kwenye zile zenye wanafunzi wa mahitaji maalumu ikiwamo Buhangija ili kupunguza tatizo hilo na wanaendelea kusubiri mchakato huo uanze kufanyiwa kazi.

"Buhangija Jumuishi inafundisha wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali, viziwi wapo 85, wasioona 22, wenye ualbino 116. Walimu waliopo kwa shule nzima ni 19, mahitaji 29 na upungufu walimu 10, kwa upande wa walimu viziwi wapo watano, mahitaji 13 na upungufu nane, walimu wa wasioona ni watano na jitihada za kutatua changamoto hii ya upungufu wa walimu inaendelea," anaongeza Mdagata.

Akizungumzia miundombinu ya madarasa na vyoo, anasema awali kulikuwa na madarasa 15 na vyoo vitano lakini kwa kushirikana na wadau, wameongeza miundombinu hiyo na kufikisha madarasa 23 na matundu 16.

"Katika ujenzi wa madarasa na vyoo, tumezingatia kuweka miundombinu rafiki kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu, ili kupita kwa urahisi kuingia darasani, pamoja na huduma za chooni," anafafanua Mdagata.

Aidha, anasema kwa yale madarasa 15 ya zamani yasiyokuwa na miundombinu rafiki, nayo wameyafanyia ukarabati ili yatumike na watoto wenye mahitaji maalumu.

Halikadhalika anasema vitabu vya mtaala mpya wa masomo vilivyo na machapisho ya nuktanundu vimepokelewa shuleni hapo kwa ajili, kuanzia darasa la tano hadi la saba, pamoja na kutoa vifaa vya kuongeza usikivu kwa wanafunzi wenye tatizo hilo.

Mwalimu Mkuu wa Buhangija, Fatuma Jilala, anaishukuru serikali na wadau kuendelea kutatua changamoto katika shule hiyo, ili kuweka mazingira rafiki ya kitaaluma kwa wanafunzi wenye welemavu.

Anasema, mazingira yasipokuwa rafiki ya kusoma kwa mwanafunzi mwenye ulemavu, hawawezi kufanya vizuri kwenye masomo yake.

Anafafanua ili mwanafunzi mwenye ulemavu apate kuelewa vizuri masomo yake, lazima vitabu vyenye alama ya nukta nundu viwepo vya kutosha pamoja na vya kuongeza usikivu kadhalika walimu wenye taaluma maalum.

"Tatizo la sasa ni upungufu wa walimu maalum, lakini serikali imeahidi kulifanyia kazi, pamoja na sisi wenyewe tunaendelea na jitihada za kuhakikisha walimu wasio na taaluma maalum wanafahamu angalau lugha za alama, ili nao wawe wanafundisha wanafunzi wenye ulemavu na kupunguza ukubwa wa tatizo liliopo," anaongeza Jilala.

Masanja Wiliam ni Mwalimu wa Buhangija ambaye anafundisha wanafunzi wenye ulemavu, anasema shule inapokuwa na zana za kutosha za kufundishia wanafunzi hao, pamoja na miundombinu rafiki inachangia kutoa elimu bora na kufanya vizuri kwenye masomo yao.

Anasema, awali walikuwa wakipata shida kufundisha wanafunzi hao wenye ulemavu kutokana na ukosefu wa nyenzo za kufundishia hasa vitabu vya nukta nundu, lakini kwa sasa vipo vya kutosha na mashine ya kuchapisha maandishi hayo inayotumiwa kutunga mitihani ya majaribio.

Mwanafunzi Pactamed Mwita, anampongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuipatia shule mashine ya kuchapisha maandishi ya nuktanundu, vifaa vya kupima usikivu hafifu kwa viziwi, pamoja na miwani ya kuongeza ukubwa wa maandishi wenye ualbino.

Diwani wa Kata ya Ibinzamata Ezekiel Sabo, anasema juhudi kubwa zimefanyika kufanikisha kuboresha mazingira rafiki ya wanafunzi wenye ulemavu shuleni hapo ikiwamo kupitia kwenye vikao vya Baraza la Madiwani.

Anasema kwa kutatua changamoto za wanafunzi hao wenye ulemavu shuleni hapo, ikiwamo uboreshaji wa miundombinu rafiki, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia, likiwamo na tatizo la upungufu wa walimu maalum ni juhudi za kipekee zilizofanywa na serikali.

"Nitahakikisha wanafunzi wenye ulemavu wanapata elimu sawa kama watoto wengine ambao hawana ulemavu, na pale penye changamoto nitapiga kelele sana, lengo watoto hawa watimize ndoto zao na kujitegemea katika maisha yao," anasema Sabo.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) mkoani Shinyanga Richard Mpongo, ambaye naye anatatizo la uoni hafifu, anasema taaluma yake ni ualimu, na ili mwanafunzi mwenye ulemavu afanye vizuri, lazima kuwapo na nyezo za kufundishia, miundombinu iwe rafiki, pamoja na walimu wa kutosha.

Anasema, kufundisha wanafunzi wenye ulemavu hakuhitaji ubabaishaji sababu ya hali zao, linahitajika umakini wa hali ya juu ili waelewe na ndiyo maana lazima kuwapo na zana zote za kufundishia yakiwamo machapisho au vitabu vya nuktanundu.

Shule ya Msingi Buhangija Jumuishi, ilianzishwa mwaka 1960 na kusajiliwa rasmi ilipofika 1974 na kuanza kutoa elimu kwa wanafunzi wasioona na viziwi, na mwaka 2009 ilianza kupokea wanafunzi wenye ualbino na kujengwa kambi jirani na shule hiyo ili kuwalinda dhidi ya mauaji.

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# 'Vijiji vinapoamua kujijengea Chuo cha VETA'

## ■Vijana takribani 400 kunufaika kitaaluma



Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Judith Nguli (kulia), akimkabidhi Meneja wa VETA Kanda ya Kusini, Neema Mwakalukwa, mkhutasari wa wananchi kuhusu maamuzi ya kutoa eneo la kujenga VETA. **MPIGAPICHA WETU**

WANAFUNZI waliokuwa wanahitimu darasa la saba na kidato cha nne, lakini wasijue pa kukimbilia baada ya kukosa nafasi za kuendelea zaidi, wamepata mkombozi kufuatia wanavijiji kutoa eneo na kujenga Chuo cha Mafunzo ya Ufundi (VETA).

Wanaonufaika ni vijana wa Vijiji vya Makata na Mitawa A, vilivyoko wilayani Liwale mkoa wa Lindi, baada ya wanakijiji kutoa ekari 50 kujenga Chuo cha VETA, kuwawezesha vijana wilayani humo kupata ujuzi wa fani mbalimbali.

Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Liwale, James Milanzi, anasema kila mwaka wanafunzi kati ya 700 na 800 wanahitimu kidato cha nne kati yao ni 200 au hadi 300 pekee wanaoingia kidato cha tano.

Anasema hayo baada ya vijiji vya Makata na Mitawa A, kutoa ekari 50 kufanikisha juhudi hizo za kuwa na Chuo cha VETA akisema mikakati ya ujenzi itawezesha vijana wengi wa kike na wa kiume kujifunza ufundi wa fani mbalimbali ikiwamo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

"Kimsingi hatua zilizochukuliwa na wananchi hawa kwa kushirikiana na serikali za vijiji inaonyesha ni jinsi gani wanajali elimu, hivyo nasi tupo pamoja nao ili kuhakikisha chuo kinajengwa," anaahidi Milanzi.

Anapongeza jitihada hizo akisema mwanafunzi anaweza kufanya vibaya katika mitihani ya mwisho, lakini akipelekwa VETA anapata ujuzi wa kumwezesha kujiajiri au kuajiriwa sehemu yoyote.

"Ninaamini kwamba, chuo hicho ni fursa hata ya wale wanaopata sifuri katika mtihani wa kidato cha nne kuweza kujiunga kwa ajili ya kupata ujuzi, kuliko kushindwa mitihani ya mwisho na kukaa nyumbani bila kujiongeza au kujiendeleza," anasema.

**MAAMUZI YA VIJIJI**

Ili kutimiza lengo hilo viongozi wa Makata na Mitawa A wamekabidhi mukhtasari wa makubaliano kati ya uongozi na wananchi na kuufikisha kwa Mkuu wa Wilaya ya Liwale Judith Nguli, anayeukabidhi kwa Meneja wa VETA Kanda ya Kusini, Neema Mwakalukwa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mitawa A, Ahmad Mchijila, anasema, wamekubaliana na wenzao wa Makata kutoa ardhi hiyo bila masharti ili kusaidia vijana wa vijiji hivyo na wilaya kwa ujumla kupata kituo cha kufundisha elimu ya ufundi.

"Awali eneo hili tulilotoa lilikuwa ni shamba la ushirika ambalo wanavijiji vyote tulikuwa tunalima kwa pamoja mazao mbalimbali, lakini sasa tumekubaliana kubadili matumizi ili kujenga Chuo cha VETA," anasema Mchijila.

Katika ufafanuzi wake anasema, sehemu ya ardhi hiyo walikuwa wameshaanza kujenga majengo mawili kwa ajili ya sekondari, lakini wameamua kuongeza ardhi zaidi kwa ajili ya VETA.

"Tumeacha na mpango wa kujenga sekondari ya wasichana, kwa kuwa ipo nyingine ya wasichana ya Anna Magoha katika Kata ya Mangirikiti ambayo ni jirani na kijiji chetu, hivyo wanakwenda kusoma huko," anasema.

Anaongeza kuwa, hata kwenye kata yao ya Makata ipo sekondari, hivyo sasa nguvu kubwa wameona ni bora kuelekeza kwenye ujenzi wa VETA, ili kuwasaidia vijana wa vijiji hivyo na wilaya kwa ujumla kupata ujuzi.

Mtendaji wa Kijiji cha Makata, Zubeda Nanjinji, anasema, majengo mawili yaliyopo sasa yalijengwa kwa nguvu za wananchi wa vijiji hivyo viwili kuanzia msingi hadi linta kwa kushirikiana na Mbunge wa Liwale Zuberi Kuchauka.

"Mbunge wetu alitupatia mifuko 50 ya saruji, mabati 100 na Sh. milioni 20 kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Sasa tunasubiri serikali kuongeza mengine zaidi kwa ajili ya VETA," anasema Zubeda.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Judith Nguli, anasema ujenzi utaanza mwakani na kwamba wakati wakisubiri wana mkakati wa kutumia majengo hayo mawili ya kwanza kuanza kutoa mafunzo.

"Tunaendelea kuwasiliana na watu wa VETA kuona uwezekano wa kuweka karakana ya ufundi wa fani mbalimbali kwenye majengo hayo ili baadhi ya vijana waanze masomo," anasema Judith.

Anaongeza kuwa kusubiri hadi mwaka wa fedha ujenzi uanze rasmi, ni mbali, na kwamba wakati wakiendelea na mchakato huo na pia kupata hatimiliki ya ardhi kuwa ya VETA, wataanza kutumia majengo hayo mawili yaliyojengwa na wananchi.

"Hivi karibuni tulifanya tamasha la 'Chomoza na Liwale' kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji tukaalika wadau mbalimbali wakiwamo wa elimu, ambao wamefika hadi eneo lilitengwa kujengwa VETA," anasema na kuongeza kuwa wanategemea watakuwa pamoja nao.

Meneja wa VETA Kanda ya Kusini, Neema Mwakalukwa, akiwa kwenye eneo hilo lililotengwa kujengwa chuo anasema, utoaji wa ekari hizo ni wazi kwamba wananchi hao wanahitaji chuo hicho.

"Chuo kikishajengwa na kukamilika kitasaidia watu mbalimbali wakiwamo vijana na watu wazima kupata elimu ya ujuzi wanaotaka, hasa kwa kuzingatia kwamba mafunzo ya VETA hayachagui umri," anaahidi Neema.

Meneja huyo anasema, mkhtasari wa taarifa za makubaliano ya wanavijiji hao ataufikisha kwa viongozi wa mamlaka hiyo ili kuweka mikakati ya ujenzi wa chuo ikiwamo kutathmini gharama zake.

Serikali ilitangaza mkakati wa kujenga vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) kila wilaya ili kutoa elimu ya ujuzi maalum kwa vijana katika maeneo mbalimbali ikiwamo utaalamu wa TEHAMA, ufundi umeme, makenika na ushonaji na utalii.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, anasema katika moja ya ziara yake ya ukaguzi moja ya vyuo hivyo, kuwa serikali inataka vijana wengi zaidi wapate mafunzo ya ufundi stadi.

Katika ufafanuzi wake, Naibu Waziri huyo anasema, katika awamu ya kwanza wanajenga vyuo vya VETA 29 na vitagharamu zaidi ya Shilingi bilioni 48.6 hadi kukamilika na kwamba watasimamia ujenzi huo kwa weledi na umakini mkubwa.

Anataja baadhi ya maeneo ambayo vyuo vimejengwa kuwa ni vya Wilaya za Nkasi, Ileje, Newala, Muleba, Kasulu, Itilima, Ngorongoro, Kongwa, Ruangwa, Nyasa na Halmashauri ya Mji wa Kasulu.

Kuwapo kwa VETA zenye karakana za fani mbalimbali, zikiwamo za ufundi umeme, useremala, uashi, ufundi bomba na uchomeleaji vyuma, kunaelezwa kuwa ni kunaongeza fursa za ajira kwa vijana.



Moja ya majengo yaliyojengwa na wananchi kwa ajili ya VETA: **MPIGAPICHA WETU**



## CBE, Chuo cha Ualimu Mpwapwa wakubaliana

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimeingia makubaliano na Chuo cha Ualimu Mpwapwa mkoani Dodoma kuanza kutoa shahada za ualimu wa masomo ya elimu ya biashara.

Aidha, makubaliano hayo yatasaidia kukabiliana na uhaba wa walimu wa masomo ya elimu ya biashara nchini katika shule za sekondari.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Emmanuel Mjema, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma wakati alipokuwa akitoa hotuba yake kwenye mahafali ya 56 ya chuo hicho.

Alisema programu hiyo itasaidia kuwapo kwa ongezeko la idadi ya walimu wa masomo ya elimu ya biashara nchini.

Kadhalika, alisema kutokana na serikali kuweka mazingira rafiki ya ufanyaji biashara na uwekezaji chuo hakina budi kutafuta naana ya kusaidia uwapo wa walimu wa kutosha katika masuala ya biashara.

Aidha, alisema pamoja na kuwapo kwa mpango huo, lakini bado chuo hicho kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa wahadhiri.

"Chuo hivi sasa kinao wahadhiri 50, lakini 21 wapo masomoni ndani na nje ya nchi idadi hii haikidhi mahitaji ya wanafunzi 1,520 waliopo hivi sasa," alisema Prof. Mjema.

Alisema changamoto nyingine ni uhaba wa hosteli pamoja na kumbi za mihadhara hali inayosababisha msongamano wa wanafunzi.

"Lakini hivi sasa tupo katika mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya ujenzi wa hosteli za wanafunzi katika eneo la Medeli west ambazo zitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi zaidi ya 1,800," alisema Prof. Mjema.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Ashil Twalib Abdallah, alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kukiwezesha chuo hicho kufikia malengo yake.

Aidha, alisema kutokana na mahitaji ya walimu wa elimu ya biashara nchini chuo hicho hakina budi kuharakisha mchakato wa makubaliano na Chuo cha Ualimu Mpwapwa kuanza kutoa shahada hizo za walimu wa elimu ya biashara.

Hata hivyo, alikitaka chuo hicho kuanzisha kozi za masuala ya uwekezaji katika sekta ya mafuta na gesi na usimamizi wa reli pamoja na kilimo biashara ili kuwezesha nchi kutekeleza azma yake ya kufikia uchumi wa viwanda.

# Tanzania yatajwa kuwa kinara kwa amani EA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema kuwa Taarifa ya Global Peace Index ya mwaka 2020 imeitaja Tanzania kuwa ni nchi ya kwanza kwa amani na utulivu kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na ya saba katika nchi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alibainisha hayo wakati alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya wizara hiyo katika kipindi cha miaka 60, ya uhuru wa Tanganyika.

"Ndugu wanahabari, ninatoa rai kwenu na kwa Watanzania wote kuendeleza amani, umoja na mshikamano uliodumu kwa kipindi cha miaka 60 iliyopita,"alisema Balozi Mulamula.

Aidha, alisema serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, itaendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano huo sambamba na kuendelea kutetea, kulinda na kudumisha usalama na amani duniani kwa kushirikiana na jumuiya ya kimataifa.

"Ushiriki wa nchi yetu ndani ya jumuiya na taasisi za kimataifa katika miongo sita iliyopita umekuwa wa mafanikio ambapo Tanzania imekuwa mstari wa mbele kupaza sauti na kuishawishi jumuiya ya kimataifa katika masuala mbalimbali yenye maslahi kwa Taifa letu na dunia kwa ujumla," alisema.

Alisema mwaka 1972 Tanzania iliungana na baadhi ya nchi zinazoendelea kuzishawishi nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuirejeshea nafasi ya kudumu Jamhuri ya Watu wa China katika Baraza la Usalama la Umoja huo ilipokuwa imeitwaa Taiwan.

Vilevile, alisema Tanzania kupitia ushirikiano wa nchi za Kusini (South South Cooperation), imekuwa ikikemea mifumo kandamizi ya kiuchumi na kisiasa na kutetea haki na usawa kwa nchi zote.

"Aidha, kupitia ushirikiano huo, Tanzania imeendelea kuzitaka nchi zilizoendelea kuheshimu ahadi zao za kutoa asilimia moja ya utajiri wao kuzisaidia nchi zinazoendelea kujikwamua na umaskini," alisema. Alisema katika kuendeleza msimamo huo wa kutetea haki na usawa kwa nchi zote ulimwenguni, katika miaka ya hivi karibuni Tanzania imekuwa mstari wa mbele kuitaka jumuiya ya kimataifa, hususani nchi za magharibi, kuiondolea Zimbabwe vikwazo vya kisiasa na kiuchumi.

"Sambamba na hilo, Tanzania imeweka bayana msimamo wake wa kupinga ukandamizaji unaofanywa kwa nchi mbalimbali duniani ikiwamo Cuba na mataifa ya Saharawi ya Magharibi na Palestina," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Bahi, Kenneth Nollo (mwenye kofia), akishirikiana na wananchi wa Kijiji cha Msisi Juu kuchimba msingi wa ujenzi wa chumba cha ofisi ya kijiji hicho, Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma juzi. Katika ujenzi huo mbunge huyo amechangia mifuko 60 ya saruji, matofali 1,200 na fedha za kulipa mafundi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Walimu waelekezwa utaratibu wa ukataji rufani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Mkwama, amewataka walimu nchini walio katika utumishi wa umma kukata rufani katika Tume hiyo wanapopewa adhabu kutokana na kufanya makosa mbalimbali.

Lengo la ushauri huo ni kuziwezesha rufani zao ziweze kushughulikiwa.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu majukumu ya TSC kwa njia ya mtandao, katibu huyo alisema kuwa mwalimu aliye katika utumishi wa umma anapoona hajaridhika na adhabu iliyotolewa na mamlaka yake ya nidhamu ngazi ya wilaya, anapaswa kukata rufani makao makuu ya TSC ambapo akiona hajaridhika anapaswa kukata rufani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya walimu wanapoadhibiwa na mamlaka zao za nidhamu badala ya kukata rufani na kwa kufuata taratibu zilizopo, wanaenda kutoa malalamiko yao kwa vyombo ambavyo havihusikinao.

"Kama mwalimu ameadhibiwa na mamlaka yake ya nidhamu ngazi ya wilaya anapaswa kukata rufani Makao Makuu ya TSC, lakini akiona hajaridhika na uamuzi uliotolewa na makao makuu anayo haki ya kukata rufani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na siyo kwenda kulalamika mahali popote anapoamua yeye," alisema Mkwama.

Aidha, alisema moja ya jukumu la TSC ni kuwasimamia walimu walio katika utumishi wa umma katika masuala mbalimbali yakiwamo ya kinidhamu, huku akibainisha baadhi ya makosa ambayo yanaweza kumtia mwalimu hatiani kuwa ni mwalimu kukataa uhamisho, kutoripoti kazini, kufanya vitendo vya ukatili kwa watoto, kung'ang'ania kituo cha awali, kushindwa kutekeleza majukumu aliyopewa na mwajiri wake na uzembe kazini.

Mkwama, alisema kwa mwalimu anayebainika kufanya makossa mbalimbali anaweza kupewa adhabu mbalimbali ikiwamo kushushwa cheo, kushushwa mshahara ama kufukuzwa kazi.

Akizungumzia kuhusu maadili ya mwalimu, alisema anapaswa kuwa katika haiba nzuri inayoendana na maadili ya ualimu katika mavazi na mwonekano wake wa ujumla.

Alisema nidhamu kwa walimu ni kitu cha msingi ili kufundisha maadili mazuri kwa wanafunzi wa ngazi ya chini.



# TORITA yaja na mbegu za kisasa za tumbaku Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

TAASISI ya Utafiti wa Tumbaku Tanzania (TORITA), imesema imegundua aina tatu mpya zenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya tani mbili kwa hekta moja, ambazo zinadaiwa kuwa zitaongeza tija kwenye uzalishaji wa zao hilo na kuwaongezea wakulima kipato.

Mwenyekiti wa Bodi ya TORITA, Prof. Gration Rwegasira, aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na wakulima wa tumbaku wa Wilaya ya Chunya kwenye mkutano uliofanyika Kijiji cha Mtanila wilayani humo eneo ambalo uzalishaji wa mbegu hizo utakuwa unafanyikia.

Alizitaja mbegu hizo ni K.326, GR. 17 na TRD 17 ambazo alisema zimeshaoteshwa na zitazisambaza kwa wakulima katika nchi nzima msimu wa kupanda utakapofika huku akiwataka wakulima kujiandaa kupanda mbegu hizo.

Alisema mbegu hizo zimefanyiwa utafiti na zimebainika kuwa ni bora kuliko zingine zilizokuwa zinatumika awali kutokana na kuzaa sana na kuwa na uwezo mkubwa wa kuhimili magonjwa pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

"Watafiti wetu wamefanya kazi kubwa sana kwenye utafiti wa mbegu hizi, sasa nawasihi wakulima mjipange kuzitumia mbegu hizi kwa msimu huu na hizi ndizo tunazoanza nazo lakini zipo zingine ambazo tutakuja nazo baadaye utafiti utakapokamilika," alisema Prof. Rwegasira.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TORITA, Dk. Jacob Lisuma, alisema serikali imetenga Sh. milioni 300 kwa ajili ya kuendeleza kituo hicho cha utafiti wa Tumbaku cha Mtanila ili kuwasaidia wakulima kuendeleza zao hilo.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha zao hilo linaendelezwa na linalimwa kisasa kwa madai kuwa ni miongoni mwa mazao yanayoliingizia taifa fedha nyingi za kigeni kutokana na mauzo ya nje ya nchi. Alisema wanakusudia kukipanua zaidi kituo hicho ili kizalishe mbegu ambazo zitatosheleza mahitaji ya wakulima wa zao hilo nchi nzima pamoja na kuongeza utafiti wa mbegu zingine zenye ubora.

"Hili jukumu tulilopewa la kusimamia kituo hiki ni muhimu sana kwa hiyo tutahakikisha tunalitekeleza vizuri kwa ajili ya maendeleo ya zao hili, tutashirikiana na wakulima kuhakikisha tunatimiza azma hii ya serikali," alisema Dk. Lisuma.

Baadhi ya wakulima wa tumbaku wa Kijiji cha Mtanila waliomba serikali kuwasaidia kupata wanunuzi wa uhakika wa zao hilo wakidai kuwa soko la zao hilo ndio tatizo kubwa kwao kutokana na baadhi ya wanunuzi kutokuwa waaminifu.

Uswege Kyamba alisema wakulima wa zao hilo wana uwezo mkubwa wa uzalishaji lakini wanakwamishwa na wanunuzi ambao huwa wanaweka ukomo wa uzalishaji wa zao hilo.

Alisema hali hiyo huwa inawalazimisha wakulima kuzalisha kwa kuzingata jitihada zao za kuongeza tija kwenye kilimo cha zao hilo, zinakwamishwa na wanunuzi wa tumbaku ambao hupanga kiwango cha ukomo wa kuzalisha zao la mahitaji.

Aliiomba serikali inapowasaidia kuboresha kilimo cha zao hilo pia iwasaidie kupata masoko ya uhakika tofauti na ilivyo sasa hivi ambapo huwa wanashindwa kufikia malengo yao.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kulia), akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, ambayo kitaifa yatafanyika jijini Mbeya, katikati ni Mkurugenzi wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Idadi wanaofeli kidato cha 4 Rungwe inatisha

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

KATI ya asilimia 60 na 70 ya wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya wanaambulia madaraja ya nne na sifuri, hali ambayo inaifanya wilaya hiyo kushika nafasi za chini katika uwiano wa kielimu mkoani humo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, wakati wa hafla ya uzinduzi wa Shule ya Wasichana ya Joy Sekondari iliyopo katika Kata ya Ntokela wilayani humo ambayo inamilikiwa na mtu binafsi.

Mkuu huyo wa Wilaya alisema alibaini hali hiyo kufuatia utafiti alioufanya yeye binafsi kwa kushirikiana na Ofisa Elimu wa Wilaya hiyo, na kwamba utafiti huo ulihusisha miaka mitatu ambayo ni kuanzia 2018 mpaka 2020.

Alisema katika utafiti huo walibaini kuwa wanafunzi wengi hawafaulu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo idadi kubwa ya wanafunzi hao kuwa wenyeji wa wilaya hiyo na hawana mchanganyiko na wenzao wa kutoka nje ya wilaya.

Dk. Anney alisema utafiti huo pia ulihusisha ufuatiliaji wa somo moja moja, na kwamba walibaini pia ufaulu uko chini hasa kwa masomo ya Sayansi.

"Katika kipindi cha miaka mitatu ni mwanafunzi mmoja pekee kati ya wanafunzi 10,000 ndiye aliyefaulu somo la Fizikia kwa kupata alama 'A' na somo la Uraia ni wanafunzi saba pekee ndio waliofaulu kwa kupata alama 'A', " alisema Dk. Anney.

Alisema masomo ambayo angalau wanafunzi wameonekana kufanya vizuri ni Kiswahili ambacho wanafunzi 253 walifaulu kwa kupata alama 'A', Kiingereza wanafunzi 230, Kemia wanafunzi 63, Biolojia wanafunzi 59, Historia wanafunzi 18 na Jiografia wanafunzi 10.

Alisema baada ya kubaini tatizo hilo wataendelea kuwashirikisha wadau wengine wa elimu katika wilaya hiyo wakiwamo walimu na wazazi ili kuandaa mpango wa pamoja wa kuinua kiwango cha ufaulu kwenye maeneo yote kuanzia somo moja moja mpaka ufaulu wa jumla.

Akifungua shule hiyo, Mwenyekiti wa Unioni ya Kusini mwa Tanzania ya Kanisa la Waadventista Wasabato, Mark Malekana, alisema tatizo linalosababisha ufaulu wa wanafunzi katika wilaya hiyo kuwa chini ni usimamizi hafifu.

Alisema ili kuondokana na tatizo hilo ni lazima kuwe na ushirikiano wa pamoja kati ya wadau wote wa elimu wilayani humo kuanzia walimu, wazazi na viongozi wa serikali na kwamba kila mmoja anatakiwa kutimiza wajibu wake ipasavyo.

Aliwataka wazazi kuhakikisha wanafuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni badala ya kuwaachia walimu pekee kufanya kazi hiyo akidai kuwa hawawezi kuondokana na tatizo hilo.

Meneja wa Shule hiyo, Augustino Mzava, alisema shule hiyo imeanzishwa kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike kusoma katika mazingira rafiki yatakayowawezesha kufaulu kwa kiwango kinachoridhisha na kwamba wanawalea wanafunzi hao kielimu na kiroho.

## Walalamikia bei kubwa ya mbolea

**Na Naebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa Kata ya Ikukwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo ili bei za bidhaa hizo zipungue kwa madai kwa kwa sasa bei ya mbolea haishikiki.

Wakizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki wananchi hao walisema kwa sasa mbolea ya kupandia mfuko wenye ujazo wa kilogramu 50 wananunua kwa bei ya Sh. 115,000 bei ambayo walidai wanashindwa kuimudu.

Mmoja wa wakulima hao, Joseph Shila, alisema kutokana na bei ya mbolea kuwa juu, wakulima wengi watashindwa kuzalisha mazao ya kutosha na hivyo kuna uwezekano baadaye ikatokea njaa.

Alisema miaka ya hivi karibuni mfuko wa mbolea ya kupandia walikuwa wananunua kwa bei ya kati ya Sh. 55,000 na 65,000 lakini kwa sasa bei imepanda mara dufu hali ambayo inawapa wakati mgumu wa kuendelea kulima.

"Tunaiomba serikali angalau iweke mkono wake kwenye mbolea, hivi sasa naamini wakulima wengi tutarudi kwenye kilimo cha asili cha kutotumia mbolea jambo ambalo nina uhakika tija haitakuwapo na tunaweza baadaye tukakumbwa na njaa," alisema Shila.

Alisema kwa sasa ardhi imeshazoea matumizi ya mbolea na kwamba endapo watapanda mazao bila kutumia mbolea kuna hatari wasipate kabisa mavuno.

Naye Neva Kanji alisema wakulima wengi sasa hivi wameanza kununua mbolea za asili ikiwemo samadi ili angalau kupunguza makali ya bei ya mbolea na kwamba nayo imeanza kupanda bei kutokana na wafugaji kuona fursa.

Alisema awali walikuwa wananunua kwa kukadiriana lakini sasa hivi wafugaji wamekuja na vipimo ikiwamo mifuko na kukadiria magari ya kubeba mchanga.

Alisema pamoja na bei ya mbolea kuwa juu, lakini hata mbegu za mahindi nazo hivyo imepanda tofauti na ilivyokuwa awali na kwamba hali hiyo inaanza kuwarudisha wakulima kwenye matumizi ya mbegu za asili.

Alisema awali mfuko wa kilogramu mbili za mbegu za mahindi walikuwa wananunua Sh. 11,000, lakini sasa hivi zimepanda na zinauzwa Sh. 12,000.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema ofisi yake inakusudia kukutana na wafanyabiashara wa pembejeo wa mkoa huo ili kujadiliana nao namna ya kupunguza bei ya mbolea ambayo imeonekana kuwa mwiba kwa wananchi.

Alisema tatizo la bei ya mbolea kupanda ni la dunia nzima, na kwamba limesababishwa na mlipuko wa corona ambao ulisababisha viwanda vingi kusitisha uzalishaji.



## Mazingira bustani ya manispaa kulimwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Chuo Kikuu cha Postdam cha Ujerumani, Prof. Oliver Gunther, amesema ushirikiano uliopo na Manispaa ya Mjini utasaidia kuhifadhi na kudhibiti mazingira ya bustani ya Botanic Migombani Mjini Zanzibar.

Prof. Oliver amesema kwamba ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake akiwa na ujumbe aliyofuatana nao alipotembelea katika bustani hiyo na kuangalia uhifadhi wa mazingira na kupata fursa ya kupanda miti mbalimbali ya kiasili ikiwamo miti iliopotea katika bustani hiyo.

Alisema uhifadhi wa miti husaidia kuimarisha mazingira pamoja na kudhibiti wanyama wengi wasipotee, jambo ambalo huipendezesha na kuipa haiba bustani hiyo.

Naye Meya wa Zanzibar, Ali Haji Haji, alisema amefurahishwa na ugeni uliowafikia kutoka Postdam Ujerumani ambao ni marafiki wao wa muda mrefu takribani miaka 10, kwa kutunza na kuhifadhi mazingira ya bustani hiyo pamoja na kufanya utafiti mbalimbali wa miti ya kiasili.

Aidha, alisema matarajio yao kutokana na ugeni huo ni kuongeza ushirikiano wa pamoja katika kuinyanyua bustani hiyo na kuirejesha miti ya asili ambayo imeshatoweka.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Mjini, Ali Khamis Mohammed, alisema Chuo Kikuu cha Postdam Ujerumani hutoa misaada mbalimbali ya kuimarisha bustani hiyo, kwa lengo la kuirejesha hadhi yake ya awali.

Aidha, alieleza Manispaa ya Mjini itaendeleza kushirikiana na wadau ili kuimarisha bustani mbalimbali zilizopo katika manispaa hiyo.

Mkuu wa Idara ya Huduma za Jamii na Mazingira, Manispaa ya Mjini, Mwanajuma Ali Abuod, aliutaka ujumbe huo kuitumia fursa hiyo kwa kufanya utafiti wa kisaikolojia ya miti katika Manispaa ya Zanzibar.

# SMZ: Tutasimamia, kuratibu vizuri shughuli za uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema serikali itaendelea kusimamia na kuratibu vizuri shughuli mbalimbali za uwekezaji ili kuboresha mazingira ya uwekezaji

Alisema hatua hiyo itasaidia kila mwekezaji ajisikie kuwa yupo sehemu salama kwa ajili ya kufanya shughuli zake na miradi aliyoielekeza kuwa katika mikono salama.

Aliyasema hayo jana Mjini Zanzibar katika hafla ya programu ya ufunguzi wa mradi ya ujenzi wa nyumba mpya zinazojengwa huko Nyamazi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja katika mji wa (Fumba Tawn) zinazojengwa kampuni ya Corporate Property Solution (CPS).

Soraga alisema kuwa kuna hitaji kubwa la nyumba kutokana na ongezeko la idadi ya watu, hivyo programu hiyo itakuwa suluhisho ya kila mmoja kupata nyumba safi na salama kwa ajili ya kuishi.

Alisema mradi huo ni pekee unaoweza kuwagusa Wazanzibari, hivyo wananchi kutokaa nyuma wala kutokuwa wanyonge, na kwamba CPS kwa kushirikiana na taasisi za kibenki zimeweka utaratibu maalum wa kuwawezesha wananchi kumiliki nyumba hizo.

"Walengwa ndio sisi Wazanzibari, hivyo tuchangamkie fursa ambazo zipo ili hatimaye tuwe sehemu ya mradi huu ambao ni kivutio duniani kote,"alisema Soraga.

Waziri huyo alisema mradi huo utatambulisha mpangilio mzuri wa makazi na kuwa na mpango mji mzuri ambapo hali ya makazi haipo vizuri.

Alisema kuwa licha ya uwepo wa changamoto mbalimbali za uwekezaji, lakini serikali kupitia mamlaka ya uwekezaji Zanzibar itaendelea kuwaunga mkono wawekezaji ili kutatua changamoto zinazowakabili.

Alieleza kuwa serikali ipo katika hatua ya kurekebisha sheria ya uwekezaji na katika kikao cha Baraza la Wawakilishi unatarajiwa kuwasilishwa mswaada wa maboresho ya sheria ya uwekezaji ili kuwashajihisha wawekezaji kuwekeza Zanzibar.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya CPS, Sebastian Dietzold, aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa ushirikiano anaupata katika ujenzi wa nyumba hizo, ambazo zitasaidia makazi kwa wananchi.

Alisema kampuni yake imeshajenga nyumba katika Kijiji cha Nyamazi ambazo kwa sasa zinaishi familia 150 na katika mradi mpya uliozinduliwa, inatarajia kujenga nyumba zingine 250 katika kijiji hicho.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, akizungumza wakati wa hafla ya programu ya ufunguzi wa mradi wa ujenzi wa nyumba mpya zinazojengwa Nyamazi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja na kampuni ya CPS. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Othman aeleza sababu ACT - Wazalendo kuingia SUK

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT- Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema chama hicho kinashiriki katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUKI) ili kuendelea na ujenzi wa msingi imara wa serikali hiyo.

Pia lengo la chama hicho kuwamo katika SUK ni kuifanya iwe bora zaidi kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo jana huko Kojani Wilaya ya Wete Pemba alipozungumza na wananchi na wanachama wa wachama hicho katika mkutano wake wa kujitambulisha rasmi kwa wananchi wa Jimbo la Kojani.

Aliwataka Wazanzibari kuendelea kuunga mkono serikali hiyo kwa kuwa ni muhimu inamanufaa sana kwa nchi na itasaidia katika kudumisha amani na mshikamano miongoni mwa wananchi, jambo ambalo linasaidia katika kujenga ustawi wa maendeleo ya taifa.

Othman alisema viongozi wa chama hicho hasa wale walioko serikalini licha ya uchache wao, watajitahidi kuhakikisha kwamba kwa ushirikiano mkubwa wanatekeleza yale yote yatakayosaidia kujenga na kuimarisha serikali hiyo iliyoasisiwa kwa juhudi za Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, ambaye alijitolea katika kusimamia amani nchini.

Alisema kwamba katika kujenga amani ya kweli katika nchi na kuleta maendeleo ni muhimu kujengwa misingi imara ya haki kwa wananchi katika nyanja tofauti ikiwamo suala la uchaguzi wa viongozi wa ngazi mbalimbali nchini.

Aliwataka wananchi kuendeleza ushirikiano na mshikamano miongoni mwa jamii kwa kuwa ndio silaha kubwa na muhimu katika kujenga amani ya kweli na kuleta maendeleo ya haraka Zanzibar. Alisema ili Zanzibar iweze kujengwa vyema, ni lazima chama hicho kiwamo katika SUK kwa kuwa kuna faida ya kuleta utulivu na kuanza safari ya kwenda mbele kimaendeleo.

Aidha, alisema licha ya chama hicho kuwa na wawakilishi wachache serikalini, lakini kazi kubwa wanayoendeleza ni ujenzi wa SUK iliyo imara, hivyo kuwepo unafuu wa kupata ushirikiano na misaada ya wahisani inayochangia kasi ya maendeleo ya Zanzibar.

Alisema hivi sasa Zanzibar imetulia na ndio maana wahisani mbalimbali tayari wamevutika na wameanza kujitolea kuisaidia fedha za kuchangia maendeleo ya taifa.

Alisema isingewezekana hivi sasa Zanzibar kupata misaada ya kimaendeleo kutoka kwa wahisani kama sio sababu ya kuwapo umoja na utulivu uliotokana na ushiriki wa chama hicho katika SUK na sasa nchi ina amani ya kweli.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Nassor Ahmed Mazrui, aliwakumbusha wananchi kuendeleza umoja na mshikamano pamoja na kuunga mkono serikali hiyo kuwa ni muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar.

Aliwataka wananchi hasa wa Kojani wampokee, Othman aendeleze mema yote yaliyoachwa na mtangulizi wake, Hayati Maalim Seif.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**CHARLES B SAMHENDA** anatangaza kupotelewa na vyeti vyake. Cheti cha FORM FOUR (CSE) kilichotolewa mwaka 2012 St.Peter's Seminary chenye Index No **S0154-0008.** Cheti cha FORM SIX ( ACSE) kilichotolewa mwaka 2015 Ilboru Secondary School chenye Index No. **S0110-0541.** Vilipotelea kwenye gari la Machame kutoka Arusha kwenda Dodoma. Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu

Taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/541416/2021. na DOD/DOD/RB/541417/2021.**

116583402

---

**JAMHURi YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**FORM II**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa mirathi NA. 103/2021**

**Ombi la MOHAMED JAWAAD LALJI AND ANOTHER kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HUSSEIN JAFFER LALJI**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 03-12-2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 22/11/2021

SAHIHI YA HAKIMU

116582102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**

**WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 59/2021**

**MDAI: CATHERINE IFRAHIM**

**DHIDI YA**

**MDAIWA FRANCIS RWECHUNGURA GABRIEL**

**WA**

**POPOTE ALIPO BARA NA VISIWANI**

**AMRI:**
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 24/11/2021 Saa 2:30 Asubuhi bila kukosa.
Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo,na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo Jumanne tarehe 16 mwezi 11,2021

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE GEITA.

116582302

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KAKULU BURCHARD KAKULU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba za usajili **T 508 CWM** chasis namba **NCP600225717** engine namba EAA5717,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/URA/RB/555082/2021**

116582902

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GALLAGHER POWER FENCE (T) LTD**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T983 AXP.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi
**ARU/KIK/RB/551094/2021.**

216581902

---

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117 R. E. 2002)**
**CHANGE OF NAMES BY DEED POLL**

**BY THIS DEED,** I the undersigned **NURU JAMES MSWAHILI of P. O. Box MWANZA, DO HEREBY** absolutely renounced and abandon the use of my former names of **NURU JAMAS MSWAHILI** appeared on my National Identity Card which is in the process for registration was mistakenly written by the responsible officers, and in lieu thereof do assume and adopt the name of **NURU JAMES MSWAHILI** appeared on my Birth Certificate with registration **No. 1558746A.**

And **IN PURSUANCE** of such changes of name as aforesaid, I hereby declare that I shall at all times hereinafter in all records, deeds and instruments and upon all occasions whatsoever, use and sign the said name of **NURU JAMES MSWAHILI** as my name of lieu of the said name of NURU JAMAS MSWAHILI.

And **I HEREBY AUTHORIZE** and request all persons to designate and address me by such assumed name of **NURU JAMES MSWAHILI** only.

**SIGNED** and **DELIVERD** by the said
**NURU JAMES MSWAHILI**
who is known to me personally/
Identified to me by ...
In my presence this ... day of ... 2021

DEPONENT

**BEFORE ME:**
**NAME:** ...
**SIGNATURE:** ...
**POSTAL ADDRESS:** ...
**QUALIFICATION:** ...



116583202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**FORM II**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya Wilaya ya TANGA**

**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa wa TANGA**

**Usimamizi wa mirathi NA. 191/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU HASSANI ISSA KIGWE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**

**MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARIAM HAMADI KIGWE**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 25 Mwezi 11 Mwaka 2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia: Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 4 Mwezi 11 Mwaka 2021.

HAKIMU MKAZI MWANZO

116583102

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SABRI R ABDALLAH**
Anatangaza kupotelewa Kwa Kadi yake ya Pikipiki yenye Plate No **MC 922 CMM,** CHASSIS No **LC6PCJK22K0084623,** ENGINE NO **156FMI-5AD2F68343.** kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Rb Namba.**
**MOR/MOR/RB/554294/2021**

116582402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**FORM II**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya Wilaya ya TANGA**

**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa wa TANGA**

**Usimamizi wa mirathi NA. 191/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU HASSANI ISSA KIGWE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**

**MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARIAM HAMADI KIGWE**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 25 Mwezi 11 Mwaka 2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia: Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 4 Mwezi 11 Mwaka 2021.

HAKIMU MKAZI MWANZO

116582002

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Anayedaiwa kuchapwa na polisi aendelea vizuri ICU

Na Romana Mallya

WAKATI Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam likichunguza tukio la askari Polisi wa Kituo cha Polisi Goba kudaiwa kumjeruhi Issa Kassim (20) kwa kipigo kituoni hapo, hali ya majeruhi aliyeko Chumba cha Uangalizi Maalumu (ICU) nayo inaendelea kuimarika, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Uhusiano wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Patrick Mvungi, ambako ndiko alikolazwa majeruhi huyo alisema mgonjwa huyo kwa sasa anaendelea vizuri.

"Bado yupo ICU lakini hali yake inaendelea vizuri," alisema.

Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro alipotafutwa na gazeti hili jana ili kujua uchunguzi wa tukio hilo umefikia wapi, alisema Jeshi la Polisi linaendelea kuchunguza hilo.

Tukio hilo lilidaiwa kutokea Novemba 10, mwaka huu kituo cha Polisi Goba baada ya kijana huyo kukamatwa na askari polisi kwa madai ya wizi wa runinga.

Novemba 16, Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi limefungua jalada la uchunguzi huku likiita malalamiko ya ndugu ni mazito.

"Kijana huyu inadaiwa alikamatwa Novemba 10, mwaka huu kwa tuhuma za wizi wa runinga na baadae kupigwa huku ikidaiwa ndugu zake walikuwa wakiombwa rushwa ili aachiwe.

"Malalamiko hayo ni mazito hivyo Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limeshafungua jalada la uchunguzi na mifumo ya kisheria itatumika ili kupata ukweli wa jambo hili na ikibainika ni kweli hatua za kisheria na za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wahusika. Uchunguzi umeshaanza." Kamanda Muliro alisema siku hiyo.

Tukio hilo liliibuliwa kupitia taarifa ya ndugu iliyosambaa katika mitandao ya kijamii Novemba 16, ikifichua madai ya ndugu yao kupigwa na askari hadi kulazwa ICU na kudai polisi kutaka fedha ili wamuachie.

Sehemu ya taarifa hiyo ilidai kijana huyo alikamatwa na polisi nyumbani kwao Goba baada ya kuuziwa runinga ya wizi, tukio ambalo ndugu hao walidai mtuhumiwa alilikana kulitenda.



Mkurugenzi Mtendaji wa TotalEnergies Marketing Tanzania Limited, Jean-Francois Schoepp, akihudumia gari la mmoja wa wateja wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Wateja iliyoanza jana, katika kituo cha TotalEnergys Oysterbay Service Station. Kushoto ni dereva wa gari hilo Glorious Hubbert Kilato. **NA MPIGAPICHA WETU**

## CRB yaombea zabuni kampuni za kizalendo

**Na Mwandishi Wetu,** RUFIJI

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB), imeziomba kampuni zinazojenga mradi wa kuzalisha umeme wa megawati 2,115 kuzipa zabuni ndogondogo kampuni za wazawa ili zishiriki ujenzi wa mradi huo.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Consolata Ngimbwa, wakati yeye na wajumbe wa bodi walipotembelea mradi huo ulioko Rufiji Mkoa wa Pwani.

Mradi huo ambao mpaka sasa umefikia asilimia 48 unatekelezwa na makampuni mawili ya Arab Contractors kwa pamoja na Elsewedy Electric zote kutoka nchini Misri.

Ngimbwa alisema zipo kampuni za kizalendo zinazoweza kufanyakazi kwenye mradi huo na zikaonyesha matokeo mazuri hivyo ni vyema kama watapewa zabuni ili nao washiriki kwenye ujenzi wa mradi huo.

Wajumbe hao walionyesha kufurahishwa kwao na maendeleo ya mradi huo na kujifunza mambo mengi.

"Mradi huu ni mkubwa sana na una kazi nyingi sana hivyo naona fursa zipo kwa makandarasi wazawa kupewa kazi ndogo ndogo kama sub – contractors wapeni kwa sababu wana uwezo wa kuzifanya," alisema.

Pia alizitaka kampuni zinazohusika na masuala ya ukandarasi hapa nchini kushirikiana kwenye miradi ili kuwa na nguvu ambazo licha ya kuzisaidia kupata mitaji mikubwa itawawezesha kufanya kazi kwa kipindi kifupi na ufanisi utakaoleta matokeo chanya katika mradi husika.

## CCM yaitaka NFRA mpango endelevu ununuzi mahindi

**Na Beatrice Shayo,** KATAVI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameutaka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuweka mpango utakaosaidia kununua mahindi ya wakulima kwa wakati na siyo wakati wa msimu wa mavuno.

Akizungumza mara baada ya kutembelea mradi wa ujenzi wa ghala na vihenge sita vya kuhifadhia mazao ya wakulima kanda ya Sumbawanga wilayani Mpanda mkoani Katavi, alisema ni lazima watafsiri kwa vitendo namna itakavyoleta matokeo chanya.

Alisema haitakuwa busara kuwepo na vihenge halafu baadaye wakulima walalamike pa kuuza mazao yao.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, alisema mradi huo utakamilika Machi, mwaka huu ili kuanza kupokea mahindi kutoka kwa wakulima.

Kwa mujibu wa Mrindoko, mradi huo wa Vihenge sita wenye uwezo wa kuhifadhi tani 3,300 kwa kila kimoja ulianza kujengwa Januari 14, mwaka 2019 na unatarajiwa kukamilika 31 Machi, 2022.

Akizungumza kwa niaba ya Meneja wa NFRA Kanda ya Sumbawanga, Mhandisi Mussa Chiyanda, alisema mradi huo wenye thamani ya Sh bilioni 14 mpaka sasa umetekelezwa kwa asilimia 95 kwa ujenzi wa vihenge na asilimia 80 ujenzi wa miundombinu.

Mrindoko alisema ili kuwasaidia kusukuma maombi yao kwa Wizara ya Kilimo kuidhinisha kwa haraka maombi ya mkoa wa Katavi kuwa Kanda ya Ununuzi wa Mazao ya NFRA.

Mwanamvua alisema mpango huo utasaidia wakulima wa Katavi kupata huduma ya kuuza mazao yao kwa NFRA kwa ukubwa na kwamba NFRA itakuwa karibu zaidi tofauti na ilivyo sasa.

Alisema uzalishaji wa mahindi na mazao mengine Katavi ni mkubwa na kwamba mkoa huo unafunguka kwa kasi kibiashara na kiuchumi.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Chongolo alikubali ombi hilo na kuahidi kuwasilisha kwa serikali ili kuidhinisha maombi ya viongozi wa Mkoa kuwa kanda ya ununuzi na uhifadhi wa mazao ya mahindi.

# BOCCO, FEI TOTO WATWAA TUZO MCHEZAJI BORA 2020

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Simba, John Bocco na kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto ', wameshinda Tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka 2020 wa Mashabiki zilizotolewa na Chama cha Soka Wilaya ya Ilala juzi.

Katika halfa ya tuzo hizo zilizofanyika jijini Dar es Salaam juzi, Bocco ameibuka kidedea baada ya kuwashinda mlinda mlango wa Simba, Aishi Manula na mlinzi wa kushoto wa timu hiyo, Mohammed Hussein 'Tshabalala, wakati Fei Toto akiwashinda wachezaji wenza wa Yanga, Deus Kaseke na Zawadi Mauya.

Msimu wa 2020/21 ulikuwa bora kwa nyota hao, ambapo Bocco alishinda tuzo nyingi binafsi; ikiwamo ya Mfungaji Bora wa Ligi Kuu na ile ya Mchezaji Bora wa Mwaka (MVP), huku Fei Toto akitangazwa Mchezaji Bora wa Kombe la Shirikisho la Azam.

Tuzo zingine zilizotolewa ni klabu bora za Ligi Kuu Tanzania Bara zenye asili ya Ilala zikiongozwa na Azam FC, iliyoanza kucheza ligi ya daraja la chini Ilala kabla ya kupanda Ligi Kuu na kuhamia Chamanzi, Mbagala.

Timu nyingine ni Simba iliyofanya vizuri katika ngazi ya ligi ya ndani kwa kutwaa ubingwa misimu minne mfululizo na kuwakilisha vema nchini katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuishia hatua ya robo, hivyo kuchukua tuzo hiyo ikitokea Ilala.

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, ametunukiwa tuzo ya kiongozi maalum ambaye ametoa mchango na kuufanya mpira wa Tanzania kuendelea kupiga hatua ikiwamo soka la wanawake na vijana iliyotolewa na Mwenyekiti wa IDFA, Mussa Kondo.

Tuzo zingine zilizotolewa ni mwezeshaji bora wa klabu zote za Ilala, ambayo imekwenda kwa Mbunge wa wilaya hiyo, Mussa Azan Zungu, ambaye amekuwa mdau mkubwa kwa kusaidia kulipia ada kwa timu za wilaya hiyo zinazoshiriki Ligi Daraja la Tatu mkoa.

Kwa upande waamuzi bora wa Ligi Daraja la Tatu, imechukuliwa na Shaban Ramadhani akiwashinda Said Mtitu na Raphael Charles, huku timu ya Magereza ikipewa zawadi ya ubingwa na kocha wao, Shame Gecha akiwa kocha bora wa ligi hiyo kwa mwaka 2020.

## Azam wajilaumu wenyewe kipigo KMC FC

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata ushindi wao wa kwanza msimu huu kwa kuichapa Azam FC mabao 2-1 katika Uwanja wa Uhuru juzi, Kocha Mkuu wa KMC FC, Habib Kondo, amesema sasa ndio wameanza Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kondo alisema mipango yake aliyoingia nayo katika mchezo huo ilifanikiwa kwa kupata pointi tatu ambazo zinampa nafasi ya kutembea kifua mbele kuwa sasa wameanza ligi rasmi.

Alisema hawakuanza vizuri ligi kwa msimu huu na walitumia wiki tatu za mapumziko ya kalenda ya Fifa kufanyia kazi mapungufu ya kikosi chake jambo ambalo walifanikiwa huku wachezaji wake wakionyesha kiwango kizuri.

"Wakati tukijiandaa kwa mchezo wetu dhidi ya Azam FC, niliwaambia wachezaji wangu kwamba tunaenda kuanza ligi na kusahau matokeo ya mechi tano zilizopita, tumefanikiwa kwa kutumia ubora na udhaifu wa wapinzani wetu kupata ushindi huo," alisema Kondo.

Alisema ushindi wao huo umewarudisha wachezaji wake katika morali nzuri na kuahidi sasa ni mwendo wa kutafuta pointi tatu kwa kila timu watakazokutana nazo kwenye ligi hiyo.

Naye Kocha msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema kipindi cha kwanza hawakucheza vizuri na licha ya kutengeneza nafasi nyingi za wazi, washambuliaji walipoteza umakini na kushindwa kuzibadilí kuwa magoli.

"Kipindi cha pili tulicheza vizuri, lakini KMC FC waliweza kutumia mapungufu kupata ushindi na kuondoka na pointi tatu katika mchezo huu, sasa tunasahau matokeo ya mechi hii na tunarudi uwanjani kufanyia kazi madhaifu yetu kwa kujipanga na mechi zijazo," alisema Bahati.

**MADHAMBI...**



Kiungo wa Azam FC, Mzambia Paul Katema, akimchezea madhambi mchezaji wa KMC FC kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi na kumalizika kwa Azam kukubali kipigo cha mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Baraza na dawa ya 'wapaki basi'

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, amesema kupoteza mechi ya Jumamosi kwa mabao 2-1 dhidi ya Geita Gold, kulitokana na wapinzani wao kucheza mchezo wa kujilinda zaidi maarufu kama 'kupaki basi' huku akisema atawafundisha wachezaji wake jinsi ya kutegua mitego hiyo.

Alisema baada ya wapinzani wao kupata bao la kwanza dakika za mwanzo, walirudi nyuma, kwa bahati nzuri wakapata bao la kusawazisha, lakini baada ya kufungwa la pili walirudi tena 'kupaki basi' ikawa ngumu kwao kuwafungua na kusawazisha.

"Walipaki basi, kila walipokuwa wanafunga bao, kwa maana hiyo natengeneza mfumo kwa ajili ya timu yoyote ambayo inakaa nyuma tu," alisema kocha huyo raia wa Kenya.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa Geita Gold, Fred Felix Minziro, alisema ushindi wa mabao 2-1 ambao ameupata akiiongoza timu hiyo, umetokana pia na baraka za wazee wake, kwani alipokwenda mkoani humo, alipitia kwanza kuwasalimu, timu yake ikashinda kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar.

"Nimeanza kuiongoza timu, tumekuja hapa mkoani Kagera ambako ni kwetu, nimeenda kuwasalimu wazee wangu, wamenipa baraka zao na kweli ndugu yangu nimeshinda, nimeweza kuiongoza timu kushinda kwa mara ya kwanza. Pamoja na mambo mengine lakini ni baraka kutoka kwa wazee wangu, nimefurahi sana," alisema Minziro ambaye ni mwenyeji wa mkoa huo.

Kwa matokeo hayo, Kagera Sugar inabaki na pointi zake nane kwa mechi sita ilizocheza, huku Geita Gold ikifikisha pointi tano na iko kwenye nafasi ya 13.



Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza,

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO NJIA NYEUPE UNITED
KOCHA wa Paris St-Germain na raia wa Argentina, Mauricio Pochettino, ndiye mkufunzi namba moja anayenyatiwa sana na klabu ya Manchester United ili kuchukua kazi hiyo msimu ujao. **(Mail)**

### MESSI HANA MPANGO NA BARCA
NYOTA wa PSG, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, hana mpango wa kurudi Barcelona baada ya Rais wa klabu hiyo, Joan Laporta kusema kwamba, klabu hiyo ya Hispania inaweza kumsajili raia huyo wa Argentina katika siku za usoni. **(AS)**

### HAG NAYE ATAJWA
KOCHA wa Ajax na raia wa Uholanzi, Erik ten Hag yupo katika nafasi ya pili miongoni mwa wakufunzi wanaotafutwa na Manchester United ili kuchukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer aliyetimuliwa. **(Sky Sports)**

### XAVI AMTAKA BOUNEDJAH
KOCHA wa Barcelona, Xavi ana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Algeria, Baghdad Bounedjah mwenye umri wa miaka 29 kutoka klabu yake ya zamani ya Al-Sadd ya nchini Qatar. **(Sport)**

### POCHETTINO YUPO TAYARI
MAURICIO Pochettino ambaye alikuwa kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur ameripotiwa kwamba, yupo huru kujiunga na 'Mashetani Wekundu' msimu ujao wa majira ya joto. **(Telegraph)**

### HAG HAJASIKIA CHOCHOTE
TEN Hag amejibu uvumi kwamba, atachukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer katika klabu ya Manchester United kwa kusema hajasikia ombi lolote kutoka kwa klabu hiyo. **(Manchester Evening News)**

### LOPETEGUI APELEKWA OLD TRAFFORD
WAKALA Jorge Mendes anaisukuma Manchester United kujaza pengo la Ole Gunnar Solksjaer kwa kumuajiri kocha wa Sevilla, Julen Lopetegui. Raia huyo wa Hispania ana mkataba na klabu hiyo hadi mwaka 2024, lakini Mendes ambaye anamuwakilisha Cristiano Ronaldo anamtaka kuchukua kazi hiyo kule Old Trafford. **(Manchester Evening News)**

### ENRIQUE AKANA
KOCHA wa timu ya Taifa ya Hispania, Luis Enrique amekana madai yanayomuhusisha na klabu ya Manchester United**. (Goal)**

### MOUNT ATAKIWA MADRID
REAL Madrid ina nia ya kumsajili kiungo wa Chelsea na England, Mason Mount. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, yupo katika mazungumzo na klabu hiyo kuhusu mkataba mpya, ingawa inasemekana anahisi hapendwi na huenda akajiandaa kuondoka. Klabu za Manchester City na Bayern pia zinahusishwa naye. **(Fichajes)**

### BARISIC AWANIWA VILLA
KOCHA mpya wa klabu ya Aston Villa, Steven Gerrard anataka kumsajili beki wa kushoto wa Croatia, Borna Barisic mwenye umri wa miaka 29, kutoka klabu yake ya zamani Rangers. (Daily Record)

### BENITEZ KUSAJILI WAPYA
KOCHA wa Everton, Rafael Benitez amesema kwamba, klabu hiyo itahitaji kuwasajili wachezaji wapya katika dirisha la uhamisho la Januari, huku winga wa England Demarai Gray mwenye umri wa miaka 25, akiwa mchezaji wa hivi karibuni kupata jeraha wakati wa mechi waliopoteza kwa Manchester City. **(Liverpool Echo)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SABABU ZIDANE KUKATAA KWENDA KUINOA UNITED

**Mpango wake ni kuinoa Paris St-Germain na yupo tayari kuisubiri nafasi hiyo, lakini Pochettino....**

**PARIS, Ufaransa**

MANCHESTER United imewasiliana na Zinedine Zidane kuhusu nafasi ya ukocha, lakini kwa mujibu wa vyanzo vilivyo karibu na kocha huyo wa zamani wa Real Madrid, hana mpango wa kwenda pale Old Trafford kwa wakati huu, Daily Mail limeripoti.

Ole Gunnar Soskjaer alifukuzwa pale United Jumapili baada ya kipigo cha mabao 4-1 kutoka Watford.

Zidane aliondoka kama kocha wa Real kwa kipindi cha pili, Mei mwaka huu.

Alishinda mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kutoka mwaka 2016.

Baada ya kuondoka mwaka 2018, alirudi mwaka mmoja baadaye na kushinda LaLiga na Super Cup mwaka 2020.

Chanzo hicho kimebainisha kwamba, gwiji huyo wa zamani wa Ufaransa na kiungo wa Real, Zidane, ambaye hana kazi kwa sasa, hatakuwa tayari kwenda United kwa sasa.

Amekuwa akihusishwa na mpango wa kuwanoa miamba wa Soka la Ufaransa, Paris St-Germain na yupo tayari kuisubiri nafasi hiyo itakapokuwa wazi.

Mauricio Pochettino, ambaye mara kwa mara amekuwa akitajwa kama kocha ajae wa United, kwa sasa ni kocha wa PSG na anaonekana kuaminiwa vilivyo.

## HABARI MICHEZO

MECHI KALI
HOME
AWAY
VILLARREAL
2.73 | 3.36 | 2.53
MANCHESTER UTD
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 710

# GUARDIOLA HAJASHTUKA SOLSKJAER KUTIMULIWA



**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amemtakia kila la heri Ole Gunnar Solskjaer kuhusu majaliwa yake ya baadaye, lakini amedokeza kwamba, kufukuzwa kwa raia huyo wa Norway halikuwa jambo la kushtukiza.

Ilitangazwa Jumapili kwamba, Manchester United imeachana rasmi na Solskjaer, ambaye alikuwa amesaini mkataba wa miaka mitatu kuinoa timu hiyo.

'Mashetani Wekundu' hao walipoteza kwa kipigo cha mabao 4-1 kutoka kwa Watford, na kuwaacha nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu na ikipitwa pointi 12 na vinara Chelsea.

Kipigo walichokipata pale Vicarage Road kilikuwa ni cha tano kwa United katika mechi saba zilizopita, wakitoka pia kupigwa 2-0 na Man City wiki mbili zilizopita.

"Namtakia kila la heri, lilikuwa jambo zuri kucheza dhidi yake," alisema Guardiola bada ya timu yake kushinda 3-0 dhidi ya Everton Jumapili.

"Unapokuwa kocha wa timu kama Man United unatakiwa kushinda, vinginevyo unakuwa kwenye matatizo.

"Nimekaa hapo kwa sababu tunashinda, vinginevyo angekuwa mtu mwingine ambaye angekaa hapa badala ya mimi. Natumaini siku moja tunaweza kukutana tena. Namtakia kila la heri."

# Xavi hana uhakika Aguero kustaafu



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi amesema hana uhakika na kustaafu kwa mshambuliaji wake, Sergio Aguero na kusema hajui lolote kwa sasa.

Aguero hivi karibuni aliripotiwa kuwa atalazimika kustaafu soka kutokana na matatizo ya moyo aliyonayo baada ya kushindwa kumaliza mechi dhidi ya Alaves, ambayo ndio tatizo lilionekana na kukimbizwa hospitalini haraka kwa ajili ya vipimo zaidi.

"Sijui kitu chochote, nilizungumza naye na hicho kinachosambaa si cha kweli," alisema Xavi akinukuliwa na AS.

"Sisi hatuna hizo taarifa na sijui zimetokea wapi, nimemwambia arudi atakopojisikia vizuri, na tutakapopata taarifa sahihi za daktari tutajua nini cha kufanya."

Aguero anatarajiwa kukaa nje ya uwanja kwa miezi mitatu kwa ajili ya uchunguzi na uangalizi zaidi wa afya yake na hatma yake itajulikana baada ya madaktari kuthibitisha kama hataweza kuendelea kucheza.

Xavi Jumamosi aliongoza Barcelona kwenye mchezo wake wa kwanza na kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Espanyol.

# HABARI MICHEZO



# ANCELOTTI: VIUNGO WA REAL NI BORA DUNIANI

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti ameisifia safu yake ya kiungo ya Real Madrid kuwa ni bora kabisa duniani baada ya Toni Kroos, Luka Modric na Casemiro kuiwezesha kushinda mabao 4-1 dhidi ya Granada.

Kroos alitengeneza asisti mbili, huku Modric na Casemiro wakitoa mchango mkubwa wa mabao mengine mawili Jumapili, wakati Madrid wakiifunga Granada kwa mara ya 13 mfululizo kwenye LaLiga.

Kwa mara ya mwisho Granada kupata ushindi wa nyumbani dhidi ya Madrid ilikuwa ni Februari 2013, waliposhinda 1-0 shukrani kwa bao la kujifunga la Cristiano Ronaldo.

Marco Asensio, Nacho, Vinicius na Ferland Mendy walifunga mabao hayo ya Real Madrid, lakini safu ya kiungo ndio ilikuwa bora zaidi na Ancelotti hakusita kuipongeza baada ya mchezo huo.

Baada ya Real Sociedad kutoka sare na Valencia ilimaanisha kwamba, Madrid walipaa kileleni mwa msimamo kwa tofauti ya pointi moja.

"Nini unachoweza kusema," alisema kocha wa Madrid, Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari.

"Wanacheza kwa umakini wa hali ya juu na bado ndio viungo bora kabisa duniani kwa upande wangu.

"Wanafanya kila kitu na huwa hata siwaulizi chochote kutoka kwao, wanafanya hivyo kwa urahisi tu na hiyo ni faida kubwa sana kwa klabu yetu."

# Conte afunguka ushindi Spurs



**LONDON, England**

ANTONIO Conte amekubaliana na mashabiki wa Tottenham Hotspur ambao walikuwa na hasira na kiwango cha timu yake kilichoonyeshwa kipindi cha kwanza kwenye mchezo wa ushindi wa Ligi Kuu dhidi ya Leeds United, Jumapili.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea alisherehekea ushindi wake wa kwanza baada ya kurudi kwenye Ligi Kuu England kwa mabao ya Pierre-Emile Hojbjerg na Sergio Reguilon.

Dan James alianza kwa kuipa Leeds bao la uongozi kipindi cha kwanza na Spurs walionekana kama vile wamezidiwa kimbinu.

Baadhi ya mashabiki wa Spurs walionyesha kutofurahishwa na kiwango cha timu hiyo kabla ya Hojbjerg kusawazisha na Reguilon kuunganisha krosi ya Eric Dier ya mpira wa adhabu ndogo na kupata ushindi wa 2-1.

"Ushindi ulikuwa muhimu kwa sababu tulikuwa kwenye wakati mgumu leo," alisema Conte akiiambia Sky Sports.

"Tulicheza michezo miwili tofauti kabisa na walituzidi mbinu na maarifa kipindi cha kwanza.

"Kucheza dhidi ya Leeds na dhidi ya (Marcelo) Bielsa si rahisi. tunatakiwa kuridhika. Huo ni mtazamo wangu kwa namna mambo yalivyokuwa hasa kutokana na mwanzoni mwa msimu huu.

"Tulisherehekea ushindi kwa sababu nafikiri ilikuwa ni ngumu na tulijua hilo. Nilisoma takwimu za Leeds na kipindi cha kwanza walikuwa kwenye kiwango cha juu zaidi.

"Kwa uhakika kabisa kipindi cha kwanza hatukuwa bora, tulizidiwa karibu kila sehemu."


,494,580

JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/11/21 | 18:00 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.18 | 3.30 | 3.35 |
| 02. 27/11/21 | 18:00 | Hull City vs Millwall | 2.70 | 3.09 | 2.60 |
| 03. 27/11/21 | 18:00 | Huddersfield vs Middlesbrough | 2.46 | 3.10 | 2.85 |
| 04. 27/11/21 | 20:00 | Juventus vs Atalanta | 2.22 | 3.46 | 3.12 |
| 05. 27/11/21 | 20:30 | Mallorca vs Getafe | 2.43 | 2.90 | 3.30 |
| 06. 27/11/21 | 20:30 | Cercle Brugge vs Mechelen | 2.66 | 3.45 | 2.44 |
| 07. 27/11/21 | 20:45 | Fortuna Sittard vs Groningen | 2.72 | 3.26 | 2.47 |
| 08. 27/11/21 | 23:00 | Villarreal vs Barcelona | 2.69 | 3.33 | 2.57 |
| 09. 28/11/21 | 15:30 | Nurnberg vs St. Pauli | 2.60 | 3.23 | 2.60 |
| 10. 28/11/21 | 17:00 | Brentford vs Everton | 2.38 | 3.20 | 3.05 |
| 11. 28/11/21 | 17:00 | Bordeaux vs Brest | 2.42 | 3.34 | 2.84 |
| 12. 28/11/21 | 18:15 | Espanyol vs Real Sociedad | 3.30 | 3.25 | 2.22 |
| 13. 28/11/21 | 18:30 | Maritimo vs Pacos Ferreira | 2.66 | 3.10 | 2.66 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 23 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 4935 | Welayta Dicha FC vs Ethiopia Bunna SC | 3.71 | 2.99 | 2.02 |
| 15:05 | 4929 | AL Kawkab vs AL Nahdha | 2.39 | 3.09 | 2.80 |
| 15:25 | 5533 | Najran SC vs AL Khlood | 1.67 | 3.52 | 4.63 |
| 15:30 | 1308 | Sozopol vs Maritsa Plovdiv | 2.38 | 3.17 | 2.74 |
| 15:30 | 1818 | Yantra Gabrovo vs FC Levski 2020 Lom | 1.73 | 3.37 | 4.43 |
| 15:30 | 1846 | Sama AL Sarhan vs Al-Yarmouk | 1.56 | 3.72 | 5.21 |
| 15:30 | 2767 | Pfk Botev Plovdiv II vs FK CSKA 1948 II | 2.80 | 3.09 | 2.39 |
| 15:30 | 4230 | Moghayer AL Sarhan vs Al Sareeh | 4.32 | 3.27 | 1.78 |
| 15:30 | 4947 | Al Ahli Amman vs Ittihad AL Ramtha | 2.38 | 3.04 | 2.85 |
| 16:00 | 4777 | Bugesera FC vs Gasogi United | 1.83 | 3.75 | 4.10 |
| 16:00 | 4956 | APR FC vs Rayon Sports FC | 1.43 | 4.07 | 6.39 |
| 16:00 | 5369 | Gicumbi vs Kiyovu Sports | 3.00 | 3.35 | 2.34 |
| 16:05 | 2077 | Hajer Club vs AL Draih | 2.07 | 3.20 | 3.75 |
| 16:30 | 4564 | Arema vs Barito Putera | 2.02 | 3.17 | 3.46 |
| 16:30 | 5361 | QPR U23 vs Cardiff City U23 | 2.60 | 3.61 | 2.28 |
| 17:25 | 3350 | AL Sahel SC vs Bisha FC | 2.25 | 2.64 | 3.61 |
| 18:00 | 1681 | Jimma Aba Jifar vs Dire Dawa Kenema FC | 3.86 | 3.00 | 1.97 |
| 18:00 | 2262 | Ceske Budejovice vs Sigma Olomouc | 2.16 | 3.43 | 2.90 |
| 18:00 | 3536 | CSA Steaua Bucuresti vs Universitatea Cluj | 2.24 | 3.13 | 2.99 |
| 18:00 | 4424 | Wydad Casablanca vs RS Berkane | 2.24 | 3.14 | 2.99 |
| 18:30 | 4784 | Arab Contractors vs Ismaily SC | 2.58 | 3.12 | 2.73 |
| 19:00 | 3102 | Al Hilal Riyadh vs Pohang Steelers | 1.62 | 3.62 | 4.83 |
| 20:45 | 2946 | Dynamo Kiev vs Bayern Munchen | 9.40 | 6.00 | 1.27 |
| 20:45 | 5521 | Villarreal vs Manchester Utd | 2.73 | 3.36 | 2.53 |
| 21:00 | 4299 | Coca Cola vs Enppi Club | 2.51 | 3.00 | 2.91 |
| 22:30 | 3288 | Olympique Safi vs Raja Casablanca | 4.73 | 2.99 | 1.80 |
| 22:45 | 1043 | Plymouth vs Wycombe | 2.36 | 3.29 | 2.85 |
| 22:45 | 1298 | Oxford Utd vs Fleetwood Town | 1.83 | 3.63 | 3.87 |
| 22:45 | 1619 | Coventry vs Birmingham | 1.81 | 3.44 | 4.23 |
| 22:45 | 2008 | Gillingham vs Cheltenham | 2.70 | 3.24 | 2.50 |
| 22:45 | 2141 | Morecambe vs Charlton | 3.30 | 3.39 | 2.08 |
| 22:45 | 2336 | Middlesbrough vs Preston | 2.06 | 3.24 | 3.49 |
| 22:45 | 2794 | Blackpool vs West Bromwich | 3.48 | 3.44 | 1.99 |
| 22:45 | 3226 | Burton vs Accrington | 2.03 | 3.43 | 3.38 |
| 22:45 | 3520 | Sheffield Wed vs MK Dons | 2.32 | 3.32 | 2.88 |
| 22:45 | 4358 | Dungannon Swifts vs Crusaders Belfast | 5.97 | 4.72 | 1.39 |
| 22:45 | 4624 | AFC Wimbledon vs Crewe | 1.86 | 3.53 | 3.88 |
| 22:45 | 4743 | Shrewsbury vs Sunderland | 3.39 | 3.34 | 2.06 |
| 22:45 | 5058 | Lincoln vs Portsmouth | 2.81 | 3.30 | 2.37 |
| 22:45 | 5090 | Ipswich vs Rotherham | 2.85 | 3.19 | 2.41 |
| 22:45 | 5409 | Cambridge Utd vs Wigan | 3.93 | 3.44 | 1.87 |
| 22:45 | 5635 | Nottingham vs Luton Town | 2.28 | 3.19 | 3.05 |
| 23:00 | 1162 | Bolton vs Doncaster | 1.71 | 3.64 | 4.53 |
| 23:00 | 3994 | BSC Young Boys vs Atalanta | 3.96 | 4.01 | 1.79 |
| 23:00 | 4495 | Chelsea vs Juventus | 1.65 | 3.81 | 5.21 |
| 23:00 | 4541 | Barcelona vs Benfica | 1.70 | 4.01 | 4.49 |
| 23:00 | 4677 | Sevilla FC vs VfL Wolfsburg | 1.74 | 3.69 | 4.69 |
| 23:00 | 4896 | Lille vs RB Salzburg | 2.44 | 3.40 | 2.80 |
| 23:00 | 5501 | Malmo vs Zenit St Petersburg | 3.55 | 3.70 | 1.97 |
| 23:00 | 5884 | Reading vs Sheffield Utd | 3.38 | 3.43 | 2.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Novemba 23, 2021

Nipashe




**Sababu Zidane kukataa kwenda kuinoa United**

UKURASA 21

**WAKILI MSOMI....**



Bernard Morrison, akitia saini mkataba Simba baada ya kuachana na Yanga mwaka jana.

# PABLO ABAKIZA HESABU KWA LWANGA, MUGALU

●●● Akiri Simba kusheheni vipaji, sasa ashikilia namba kikosi cha kwanza baada ya kumaliza...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Jumapili wiki hii, akitarajia kukiongoza kikosi chake kwa mara ya kwanza kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Pablo Franco, amekamilisha hesabu zake baada ya kushuhudiwa uwezo wa kila mchezaji uwanjani.

Simba itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii kuikaribisha Red Arrows kwenye mechi ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika kabla ya timu hizo kurudiana Desemba 5, mwaka huu nchini Zambia.

Timu itakayopata matokeo ya jumla katika mechi hizo mbili, itafuzu moja kwa moja hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Kuelekea mchezo huo, Pablo alihitaji kujua uwezo wa kila mchezaji na namna wanavyocheza baada ya kuiongoza timu hiyo kushinda mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu kwa kuichapa Ruvu Shooting mabao 3-1 Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Kutokana na muda mchache alionao huku akihitaji kupata matokeo, katika mchezo huo Pablo aliwaanzisha wachezaji wote waliounda kikosi hicho msimu uliopita, isipokuwa Kibu Denis pekee.

Hata hivyo, juzi kocha huyo raia wa Hispania, alihitaji mchezo wa kirafiki ambapo walicheza dhidi ya Green Warriors, na kisha kutoa nafasi kwa wachezaji ambao hawakucheza mechi hiyo ya Ligi Kuu, hivyo kupata fursa ya kumsoma kila mmoja, akiwa sasa amebakiza wachezaji wawili tu kuwaona wakicheza, mshambuliaji Chris Mugalu na kiungo mkabaji, Taddeo Lwanga ambao ni majeruhi.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Mo Simba Arena, na Simba kuibuka na ushindi wa mabao 4-0, Pablo aliwaanzisha; Benno Kakolanya, Jimmyson Mwinuke, Gadiel Michael, Henock Inonga, Kennedy Juma, Erasto Nyoni, Duncan Nyoni, Sadio Kanoute, John Bocco, Rally Bwalya na Peter Banda.

Wakati mabao katika mchezo huo yakifungwa na Banda, Duncan, Gadiel na Yusuphu Mhilu, kipindi cha pili Pablo alifanya mabadiliko na kuwaingiza Pape Sakho, Ally Salum, Ibrahimu Ajibu, Israel Patrick na Mhilu huku akiwatoa Bocco, Erasto Nyoni, Kakolanya, Bwalya, Kanoute na Banda.

Akizungumza na Nipashe, Pablo alisema, Simba ina wachezaji wazuri wenye uwezo mkubwa kisoka, hivyo anachopaswa kukifanya ni kuwaunganisha lakini pia akiwajengea kujiamini zaidi.

Pablo pia alieleza furaha yake kwa kurejea kwa wachezaji ambao walikuwa majeruhi, huku akiweka wazi kama watakuwa fiti kwa asilimia 100, ana uhakika watafanya vizuri katika mchezo ujao dhidi ya Red Arroms pamoja na Yanga.

"Nimewaona wachezaji karibu wote, naendelea kuwasoma na kutafuta muunganiko mzuri, ili kuweza kukabiliana na michezo iliyopo mbele yetu na hata dhidi ya Yanga," alisema.

Baada ya mechi hiyo ya CAF dhidi ya Red Arrows, Desemba Mosi Simba itaikaribisha Geita Gold katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechezo wa Ligi Kuu na kisha Desemba 5, itashuka dimbani nchini Zambia kurudiana na Wazambia hao kabla ya Desemba 11, mwaka huu, kuvaana na Yanga.

## Morrison aigaragaza Yanga CAS, kulipwa mil.12/-

**Na Saada Akida**

WINGA wa Klabu ya Simba, Mghana Bernard Morrison 'Wakili Msomi', ameshinda kesi dhidi ya Yanga iliyofunguliwa Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo (CAS) kwa madai kwamba aliondoka klabuni hapo akiwa na mkataba halali.

Taarifa iliyotolewa jana na CAS, ilieleza imetoa uamuzi wake katika utaratibu wa usuluhishi kati ya klabu ya Yanga na Morrison kuhusiana na uamuzi uliotolewa Agosti 12, mwaka jana na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania ambao Yanga ilikuwa ikiupinga.

Katika uamuzi huo, mkataba wa Morrison na Yanga ulionekana kukamilika Julai 14, mwaka jana. Mkataba wa pili, uliozua malumbano, ulionekana kwa haukuingiwa na Morrison na akaamriwa kulipa kiasi cha Dola za Kimarekani 30,000 alizolipwa na Yanga kuhusiana na mkataba wa pili wenye utata.

Yanga ilipinga uamuzi huo CAS na kuomba uhalali wa mkataba wa pili uthibitishwe na kwamba Morrison aagizwe kulipa fidia ya dola za Marekani 200,000 kwa klabu hiyo kwa kukiuka mkataba.

"Jopo la CAS lilisikiliza wahusika kwa kongamano la video Julai 29, mwaka huu. Baada ya mashauriano, limetupilia mbali rufani hiyo na kuthibitisha kwa ujumla uamuzi uliokuwa ukipingwa," ilieleza taarifa ya CAS.

Hata hivyo, kwa mujibu wa wakili wa Morrison, Hussein Kitta, amethibitisha kupokea barua kutoka CAS, ikisema kwamba mteja wake (Morrison) ameshinda kesi yake dhidi ya Yanga na anatakiwa kulipwa gharama za kesi.

Alisema katika barua hiyo imeeleza mbali na CAS kutupilia mbali rufani ya Yanga, imeitaka klabu hiyo kumlipa nyota huyo gharama zote kiasi cha Swiss Franc 5,000 ambazo ni zaidi ya Sh. milioni 12 za Tanzania.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >